# Nipashe

Alhamisi Julai 11, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581734

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


**Mgombea** urais TLS: Kuna tishio kugawa mawakili, alia siasa, uadui

UKURASA 2

**Mikopo** ya asilimia 10 yaiva, vikundi vyaitwa kuichukua

UKURASA 3

**Ndugu** wafariki dunia baada ya kupewa dawa za kuacha pombe

UKURASA 4




UKURASA 11

# Utata waibuka anayebaka, kuua

• **Walengwa** wakuu watoto, uchunguzi wabaini anaacha ishara... *Ukurasa 2*






Mwonekano wa soko jipya la Kariakoo, Manispaa ya Ilala jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Masharti wafanyabiashara kuingia jengo jipya Kariakoo yatangazwa

UKURASA 5

## YALIYOMO

UKURASA WA 7

### DCI AWAHAKIKISHIA WANANCHI USALAMA

MKURUGENZI wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Kamishna Ramadhani Kingai, amesema nchi kwa sasa iko salama kutokana na utendaji kazi wa maofisa wa Jeshi la Polisi ambao wanasimamia haki ...

UKURASA WA 24

### SIMBA YAACHANA NA BABACAR SARR

UONGOZI wa klabu ya Simba jana ulitoa taarifa ya kuachana na kiungo wake, Babacar Sarr baada ya kufikia makubaliano ya pande mbili...

## Mwinyi ataka uwekezaji sekta ya sukari uwe kipaumbele

UKURASA 3

**MICHEZO** **AZIZ KI AICHAGUA YANGA** UK.24

**MAONI,** UK.6

# Utata waibuka anayebaka, kuua

Na Pilly Kigome

WATOTO watatu wameuawa kwa nyakati tofauti na mmoja kunusurika kifo katika kipindi cha miezi minne katika matukio ya ubakaji wilayani Temeke, Dar es Salaam.

Uhalifu huo unazua utata kutokana na vitendo hivyo kufanywa dhidi ya watoto wenye umri unaokaribiana, hali kadhalika mahali unakotendwa.

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Sixtus Mapunda (pichani) alibainisha hayo jana alipotoa taarifa kuhusu matukio hayo.

Alisema tukio la kwanza ni la Machi 13 mwaka huu, mtoto mwenye umri wa miaka saba, mwanafunzi, kukutwa ameuawa na mwili wake kukutwa msituni Mbagala Kibondemaji B.

Mapunda alisema kuwa kabla ya tukio hilo, Machi 12, saa 11:30 jioni, mtoto huyo akiwa na mtoto mwenzake mwenye umri wa miaka sita, walitoka nyumbani kwao Mbagala Kuu, walipofika Viwanja vya Zakheim, kuna mhalifu alitokea na kumwahidi mtoto mdogo amsubiri mwenzake eneo hilo, akiahidi kuwa wanakwenda kumnunulia zawadi ya nguo na chipsi, akaondoka na mtoto mkubwa.

Katika tukio la pili, Mapunda alisema kuwa Aprili 10 mwaka huu, mtaa wa Kokoto Charambe, mtoto wa kike mwenye umri wa miaka tisa, mwanafunzi wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Kibondemaji, alikutwa amenajisiwa na kutupwa kando ya Barabara ya Kilwa, akiomba msaada.



Mkuu wa Wilaya alisema kuwa binti huyo alikuwa na wenzake wakisherehekea sikukuu ya Idd Viwanja za Zakheim, Mbagala, lakini baadaye alipotezana nao.

Wakati anawatafuta, alitokea mhalifu na kujitambulisha ni mlinzi wa eneo hilo, akamtaka waende walikokuwa wenzake, huko akamnajisi.

Tukio la tatu kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya Mapunda, ni la mwili wa mtoto uliokotwa Juni 24 saa moja usiku, eneo la Toangoma.

Mapunda alitaja tukio la nne lilitokea Julai 8 mwaka huu, saa 1:30 asubuhi, mtoto wa miaka mitano alikutwa katika jengo ambalo ujenzi wake haujakamilika huko Kibondemaji, Kata ya Mbagala Kuu.

Mkuu wa Wilaya aliwahakikishia wananchi kuwa Jeshi la Polisi linaendelea kufanya uchunguzi na litawatia mkononi wahalifu wote waliohusika na matukio hayo.

Pia aliwataka walimu wote wa shule za msingi na sekondari kutoa elimu kwa watoto jinsi ya kujilinda kwa kutokubali mtu yeyote asiyemjua kuwapa vyakula au kuwarubuni kwa vyovyote.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Temeke, John Malulu, alisema anafahamu machungu waliyonayo familia zilizokumbwa na mauaji hayo, jeshi hilo linafanya kila linalowezekana kuhakikisha watuhumiwa watakamatwa na kufikishwa katika mkono wa sheria.

# Mgombea urais TLS: Kuna tishio kuwagawa mawakili

. Akemea siasa, uadui miongoni mwao

Na Grace Gurisha

WAKILI wa Kujitegemea Sweetbert Nkuba amesema anahitaji kurejesha anachokiita "Heshima ya Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) na kuwa nguvu moja".

Amesema kuna mambo mengi yanatishia na kuwagawa mawakili kutokana na shughuli wanazozifanya.

Amesema kuna baadhi ya wenye itikadi za vyama vyao wanataka kuihamisha TLS kutoka kwenye uhalisia wake na kutaka kuifanya kuwa chama cha siasa, jambo ambalo halikubaliki.

"Ni wakati wa familia hii (TLS) kukaa pamoja," Nkuba alisema katika mazungumzo na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana wakati uzinduzi rasmi wa kampeni zake.

Wakili huyo ameomba kuchaguliwa kuwa rais wa TLS ili "kurejesha heshima ya mawakili", akifafanua kuwa imefikia hatua wakili anayefanya shughuli za jinai anakuwa adui mkubwa kwa baadhi ya mawakili wengine.

Vilevile, mgombea huyo alidai kuwa kuna watu wenye itikadi za vyama vyao wanataka kukifanya chama hicho kuwa cha siasa.

"Kila mmoja ana itikadi ya chama chake na katika itikadi hizi mtu anaweza kubadilika muda wowote akatoka chama kimoja kwenda kingine.

"Sasa, kama wanachama wa TLS tayari walikuwa na itikadi yao ya mwanzo, je nao wahame tena kufuata itikadi hiyo?" alihoji.

Wakili huyo pia aliahidi, "Nitakwenda kupambana na vishoka wote wanaobandika matangazo wakijiita mawakili, hii hali si nzuri, inafanya sifa ya mawakili kuwa mbaya," alisema Wakili Nkuba.

Alisema amelenga kusaidia vijana chipukizi ambao wamekuwa wakibaguliwa kwa kutopewa ushirikiano na mawakili wakongwe baada ya kuwa wameapishwa tayari kuwa mawakili, hivyo ataandaa ofisi itakayojumuisha mawakili wote.

Alisema TLS iliundwa kwa lengo la kuwaleta pamoja mawakili, kutetea na kusimamia haki zao bila kuangalia ukomavu au uchanga wa mtu yeyote.

Uchaguzi wa viongozi wa TLS umepangwa kufanyika Agosti 2 mwaka huu wakati wa mkutano mkuu wa mwaka wa chama hicho utakaoanza Agosti 1-3 mwaka huu jijini Dodoma.


MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
ARUSHA
UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI
SHAURI LA MIRATHI NAMBARI 12470 LA MWAKA 2024
MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA

ELIAS MAYALA BUNDALA..........................................MAREHEMU
NA
RENATUS JAMES SHINHU..........................................MWOMBAJI

TAARIFA YA KAWAIDA
(KANUNI YA 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia maombi haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 18 Mwezi wa Julai, Mwaka wa 2024.

Imewasilishwa Arusha leo tarehe 09 Mwezi wa Julai, Mwaka wa 2024.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU
ARUSHA



KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MWANZA.

SHAURI LA MADAI YA ARDHI MAOMBI NA.13549 YA 2024

TUJIJENGE TANZANIA LIMITED......................MLETA MAOMBI
DHIDI YA
SISI AUCTION MART& GENERAL BROKERS......................MJIBU MAOMBI NA1
BENJAMIN MUNGO..................................MJIBU MAOMBI NA2
EVELINA CHRISTINA KUMLAGA.........................MJIBU MAOMBI NA3
LEAH MAKWABU..................................MJIBU MAOMBI NA4

Kwa: 1.SISI AUCTION MART & GENERAL BROKERS
2.EVELINA CHRISTINA KUMLAGA
3.LEAH MAKWABU

POPOTE MLIPO.

KUITWA SHAURINI

Fahamu kwamba, shauri tajwa hapo juu ambalo nyie ni wajibu maombi namba1,3 na 4. limepangwa kusikilizwa mbele ya Mahakama hii tarehe 23/07/2024 saa 3:00 asubuhi,mbele ya Mh.Jaji **A.MATUMA.**

Hivyo natakiwa kuhudhuria Mahakamani nyie wenyewe au mwakilishi wenu siku hiyo bila kukosa. Kutokuhudhuria kwenu kutaifanya Mahakama hii iendelee na shauri hili bila uwepo wenu..

Imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 03 mwezi **Julai, 2024**

NAIBU MSAJILI
MWANZA.



TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini niliyopewa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (N.S.S.F) nitauza kwa mnada wa hadhara vitu/mali za wadaiwa wa NSSF kama ilivyoonyesha kwenye jedwali hapa chini: -

| NA. | MDAIWA | MALI HUSIKA | MNADA UTAKAPOFANY IKA | TAREHE | SIFA ZA MALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MSAJIGWA JOAB ULISAJA NA KYEMBE DITOPILE MZUZURI | SAMANI ZA MAJUMBA NI | SINZA MORI TAMBAZA MAKAO MAKUU | 25/07/2024 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI | SOFASET, VITANDA, MAGODORO, FRIJI, MEZA, TV, REDIO, NA VITU VINGINE VINGI. |
| 2 | HILDA BASIL MSOKA NA ZAITUNI HUSSEIN | SAMANI ZA MAJUMBA NI | TEMESA-DAR KEKO MADAWA GETI NAMBA 2B | 26/07/2024 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI | SOFASET, VITANDA, MAGODORO, FRIJI, MEZA, TV, REDIO, MEZA NA VITI VYA OFISI, COMPYUTA, MIZANI NA VITU VINGINE VINGI. |
| 3 | TANZANIA DAR COACH | BODI LA BASI NA VITU VIDOGO | HIFADHI ENEO LA UZALISHAJI KWAAJILI YA MAUZO NJE YA NCHI (HEPZ) | 27/07/2024 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI | BODI LA BASI KUBWA PAMOJA NA VITU VINGINE VIDOGOVIDOGO |
| 4 | DEIGU COMPANY LIMITED | SAMANI ZA OFISINI | KILIMANJARO COMMERCIAL CONFERENCE | 31/07/2024 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI | 1. NGUO ZA KIUME, 2. VIATU, 3. MIDOLI YA KUVISHA NGUO ZA KUUZA, 4. UBAO WA MATANGAZO, 5. REDIO N.K |
| 5 | ANGELA KESSY | VITU VYA DUKANI/ NGUO TOFAUTI | KILIMANJARO COMMERCIAL CONFERENCE | 31/07/2024 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI | 1. NGUO ZA KIUME, 2. VIATU, 3. 4. MIDOLI YA KUVISHA NGUO ZA KUUZA, 5. UBAO WA MATANGAZO, 4. REDIO N.K |
| 6 | GRIENFIN | VITU VYA BAR | KILIMANJARO COMMERCIAL CONFERENCE | 31/07/2024 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI | VITI, MEZA, TV, MAJIKO,FRIJI, MUSIC SYSTEM N.K |
| 7 | LEO NYAKI | VITU VYA STATIONA RI | KILIMANJARO COMMERCIAL CONFERENCE | 1/8/24 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI | PHOTOCOPY, PRINTER, MEZA YA KIOO, N.K |
| 8 | NORTHERN SAVING AND CREDIT | SAMANI ZA OFISINI | KILIMANJARO COMMERCIAL CONFERENCE | 1/8/24 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI | PRINTER, C.P.U, SAFE YA KUWEKEA VITU VYA THAMANI, PHOTOCOPY MASHINE, MEZA NA VITU VYA OFISINI N.K |
| 9 | VERYNICE | VINYWAJI NA VITU VYA BAR | KILIMANJARO COMMERCIAL CONFERENCE | 1/8/24 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI | MUSIC SYSTEM, VINYWAJI, TV, MAJIKO, VITU, MEZA. FRIJI |
| 10 | UPENDO ASUKENYE KIBONA | SAMANI ZA OFISINI | ARUSHA – MAFAO HOUSE | 3/8/24 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI | SAMANI HIZO NI PAMOJA NA ZA OFISINI NA VITU VYA DUKANI |

MASHARTI YA MNADA

Mnunuzi atatakiwa kulipa 100% ya vitu kama fenicha au vitu vyote vidogo vidogo visivyozidi milioni moja ya kiasi alichoshinda mara tu dalali atakapomtangaza kuwa mshindi.

Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% ya kiasi alichobidi ambacho kinazidi zaidi ya milioni moja na salio la 75% ni lazima alipe ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya mnada. Kiasi cha 25% kitakachokuwa kimelipwa hakitarejeshwa iwapo mshindi atashindwa kulipa salio la 75% katika kipindi cha siku 14 kuanzia tarehe ya mnada.

i. Gharama zote za kutoa vitu vilivyouzwa ni jukumu la mteja mwenyewe.
ii. Mshindi atakakabidhiwa Mali/Kitu/Vitu mara baada ya kufanya malipo kamili (100%).
iii. Ukaguzi ni siku moja kabla ya tarehe ya mnada.

KWA MAELEKEZO ZAIDI PIGA SIMU 0713 – 327 989/ 0713 508 158 AU
BARUA PEPE; info@tambazaauctionmart.co.tz AU FIKA OFISINI KWETU SINZA MORI,
BARABARA YA SHEKILANGO KARIBU NA KITUO CHA MAFUTA BIG

HABARI KITAIFA

# Mwinyi ataka kipaumbele uwekezaji sekta sukari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema uzalishaji wa sukari Tanzania ni moja ya nyenzo kuu na muhimu ya kuimarisha na kulinda usalama wa chakula, kwa kuwa ni moja ya chakula muhimu nchini.

Aliyasema hayo wakati akifungua mkutano wa wawekezaji wa sukari wa nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na Tanzania ikiwa ni mwenyeji wa mkutano huo uliofanyika visiwani hapa.

Dk. Mwinyi alisema sekta ya sukari ni kipaumbele katika kilimo cha nchi kwa kuwa viwanda vya sukari ni vitovu muhimu vya kilimo na uchumi.

Alisema uzalishaji wa sukari Tanzania kama ilivyo kwa nchi nyingine wanachama wa SADC zinazozalisha, huokoa matumizi ya fedha nyingi za kigeni kila mwaka ambazo zingetumika kuagiza nje ya nchi, kama isingezalishwa nchini.

Dk. Mwinyi alisema kwa kutambua hilo, Tanzania imeweka mazingira wezeshi kwa uwekezaji katika kilimo cha miwa na uzalishaji sukari, kutokana na hatua madhubuti zilizochukuliwa na serikali ya kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji kuleta mafanikio makubwa na kuongezeka kwa uwekezaji mkubwa wa mitaji katika sekta ya sukari na viwanda vyote nchini vinafanya upanuzi wa kilimo cha miwa na uzalishaji sukari.

"Naomba kutumia fursa ya mkutano huu kutoa rai kwa nchi za SADC kutumia fursa tulizonazo katika nchi zetu kuweka mazingira bora zaidi ya uwekezaji ili kukuza uwekezaji katika uzalishaji wa sukari," alisema.

"Ni dhahiri kuwa, kujenga mazingira bora na kuondoa vikwazo vya uwekezaji katika sekta ya sukari kwenye nchi zetu kutawezesha kustawisha zaidi masoko ya ndani ya nchi za SADC na kuongeza fursa ya biashara ya sukari katika Soko la Pamoja la Afrika (AfCFTA) na dunia kwa ujumla."

Aidha, Dk. Mwinyi alisema sekta ya sukari katika nchi za SADC na Afrika kwa ujumla, inalazimika kuzikabili changamoto kubwa ikiwamo ushindani wa kimataifa usio katika misingi ya usawa, unaochangiwa na uzalishaji wenye mchango mkubwa wa ruzuku za aina mbalimbali, na pia, ugumu wa upatikanaji.

# Mikopo 10% yaiva, vikundi vyaitwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imetangaza kuanza kutolewa kwa mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri nchini kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu nchini kwa ajili ya kuanzisha miradi ya maendeleo na kujikwamua na umaskini.

Hatua hiyo ni baaada ya kukamilisha kanuni, mwongozo na maboresho ya mfumo wa kielektroniki wa utoaji na usimamizi wa mikopo hiyo.

Hivi karibuni, katika bajeti yake kwa mwaka 2024/25, ofisi hiyo ilitangaza kurejeshwa utoaji wa mikopo baada ya kusitishwa mwaka jana kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo ubadhirifu wa mamilioni ya fedha za serikali na kuwapo vikundi hewa.

Akifungua mafunzo kuhusu utoaji na usimamizi wa mikopo hiyo kwa wawezeshaji wa kitaifa, Katibu Mkuu TAMISEMI, Adolf Ndunguru, alisema kukamilisha nyenzo hizo pamoja na vitini vitakavyowezesha utoaji wa mafunzo kwa wasimamizi na vikundi, kutasaidia ufanisi wa mikopo hiyo kuanza kutolewa Julai Mosi, mwaka huu.

"Ni maelekezo ya serikali kabla ya kuanza kutoa mikopo zikamilike nyenzo hizi, hivyo niwatake washiriki kuelewa vema ili kwenda kufundisha wengine kwa viwango vinavyokubalika," alisema Ndunguru.

Alisisitiza wawezeshaji hao kutumia mafunzo watakayoyapata kwa kuwa serikali inatarajia kuona yanatatua changamoto za tofauti ya uelewa na tafsiri ya baadhi ya vifungu vya kanuni kati ya halmashauri moja na nyingine.

Alisema kukosekana kwa utaratibu maalumu wa utambuzi na uundaji wa vikundi vinavyotarajiwa kunufaika na mikopo kulisababisha kuwapo kwa vikundi hewa.

Alisema usimamizi usioridhisha wa mikopo, ulisababisha fedha nyingi za marejesho kutorejeshwa kwa wakati.

Mkurugenzi wa Tawala za Mikoa, Beatrice Kimoleta, alisema baada ya serikali kutangaza kurejesha mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, ofisi hiyo imepitia mambo mbalimbali ikiwamo marekebisho ya Sheria ya Fedha sura 29, mapitio ya kanuni za mikopo hiyo, uandaaji wa miongozo na vitini vya mafunzo.

Alisema baada ya mafunzo hayo, wawezeshaji 840 watajengewa uwezo wa kwenda kutoa mafunzo hayo kwa kamati za uratibu wa mikopo ngazi ya mikoa, halmashauri na kata kusimamia utoaji wa mikopo ya vikundi.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

HABARI KITAIFA

# Ndugu wafariki dunia baada ya kupewa dawa za kuacha pombe

**Na Neema Husein,** KATAVI

WATU wawili wa familia moja wamefariki dunia baada ya kupewa dawa na mganga wa kienyeji ili waache kunywa pombe.

Tukio hilo limeripotiwa katika Kata ya Kazima, Manispaa ya Mpanda, mkoani Katavi, ikidaiwa kuwa vijana hao kabla ya umauti kuwakuta walikuwa wanakunywa pombe kupita kiasi, hata kuwa kero kwa familia na majirani.

Wakizungumzia tukio hilo, ndugu wa marehemu wamesema ndugu zao walikuwa wanakunywa pombe kiasi cha kuwa kama wanachanganyikiwa.

"Kutokana na mazingira hayo, sisi kama familia tulikaa tukapanga tufanye nini ili tuweze kuwaokoa tukatafuta mganga wa kwanza akaja akawatengenezea dawa, lakini ikashindikana hali ikawa ni ilele wakaendelea kunywa pombe.

"Tuliendelea kuhangaika huku na kule tukapata mganga mwingine, naye akaja kuwatengenezea. Baada ya kuwatengenezea ndipo ghafla umauti ukawa umewakuta," alidai Justin Patrick, mpwa wa mmoja wa marehemu.

Ndugu mwingine wa marehemu, Japhet Stanslaus alisema, "Ndugu zangu walikuwa wanywaji wa pombe muda mrefu, lakini wakati wanatibiwa mimi sikuwapo. Nilipigiwa simu saa tatu usiku nikaambiwa "Bwana Paulo Malimba na Dismas Malimba wameaga dunia.

"Nilipatwa na mshtuko kwa sababu nilikuwa ninafahamu, ni wazima japo muda mrefu kidogo tulikuwa hatuonani nao kwa sababu tulikuwa tunaishi maeneo tofauti.

"Nilipofika eneo la tukio, nikapewa taarifa kuwa alikuja mganga ambaye alikuwa anajaribu kuwapa dawa ya kuacha unywaji wa pombe kupindukia.

"Walipokunywa dawa hizo ikapelekea wao kuzidiwa mpaka kufikia kupoteza uhai, tukaanza kushughulika na habari za kuwasitiri ndugu zetu."

Baadhi ya majirani zao walidai kuwa vijana hao walikuwa wakinywa pombe muda wote, wanapiga kelele na kufikia hatua hata ya kuvua nguo barabarani.

Mmoja wa majirani hao, Mch. Gerald Ndegea, alidai majirani zake hao walifika nyumbani kwao Ijumaa jioni na usiku walikwenda kunywa pombe na walirejea saa saba usiku wakiwa wanapiga yowe.

"Baada ya yowe hilo, asubuhi ikabidi sisi kama majirani tukaona hii hali hatuwezi kuivumilia. Tulienda pale ili tuonane nao, basi tukakuta walengwa wenyewe wameondoka wamekwenda tena kunywa pombe.

"Baadaye tuliongea na kaka yao, naye akasema 'ngoja waje', akamwagiza mdogo wao akawafuata. Baada ya kuwaleta wakaendelea kucheza muziki, maana pombe ilikuwa bado imo kichwani.

"Tumekaa nao hapa mpaka saa 10, mimi nikaondoka kuelekea kanisani. Saa mbili niliporudi niliwakuta wamelala, ilipofika saa tatu usiku, nikasikia yowe, mama mmoja akilia ambaye ni dada yao.

"Nikaenda kuangalia 'kulikoni?' Nikakuta bajaji, nikauliza 'kuna nini?' Wakasema 'hawa watu tumemwita daktari awapime, kasema mapigo ya moyo yako mbali'.

"Wakaondoka na bajaji kwenda Hospitali ya Kazima, lakini hawakufanikiwa kufika, baadaye walirudi kabla hatujasambaa, walipofika tayari kilio kikawa kikubwa, sisi kama majirani tukaanza kushusha zile maiti kuzipeleka ndani," alisimulia Mch. Ndegea.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kazima, Flaviana Kisalala, alithibitisha kutokea tukio hilo na kusema kuwa chanzo cha kifo, kama walivyoelezwa baadaye na mamlaka za serikali, ni dawa walizopewa na mganga ili waache kunywa pombe.

"Mganga baada ya kufika pale aliwauliza majina ya pombe wanazotumia, wakasema wanatumia gongo, wanzuki na komoni, basi zile pombe zote zikatafutwa zikachanganywa kwenye chombo kimoja akachanganya na dawa ya kienyeji akachanganya na asali mbichi akaipasha kwenye moto.

"Baada ya hapo akawapa wakanywa, walipokunywa walitapika na kuendelea kuchoka hadi kupelekea umauti. Ni kweli tuna tukio hili katika mtaa wangu na leo ndio tumefanya maziko ya miili ya hao watu wawili," alisema kiongozi huyo alipozungumza na mwandishi wa habari hii.

Tayari miili ya ndugu hao imezikwa katika makaburi ya Kazima huku mganga aliyefanya kitendo hicho, akidaiwa kutokomea kusikojulikana.



Majeneza yenye miili ya Paulo Malimba na Dismas Malimba, waliofariki dunia baada ya kupewa dawa na mganga wa kienyeji ili waache unywaji wa pombe, yakiwa nyumbani kwao katika Mtaa wa Kazima, Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi Jumatatu, wakati wa ibada ya kuwaaga kabla ya maziko yaliyofanyika kwenye makaburi ya Kazima. **PICHA: NEEMA HUSSEIN**

# Mwalimu mbaroni madai kumjeruhi mwanafunzi aliyekataa somo la fizikia

**Na Restuta Damian,** KAGERA

JESHI la Polisi mkoani hapa linamshikilia Mkuu wa Shule ya Sekondari Kata ya Kasharunga, Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, Charles Mkaruka (33), kwa tuhuma za kumjeruhi kwa kumshambulia kwa viboko mwanafunzi wa kidato cha tatu, Filinet Augustino (18) kwa kukataa kusoma somo la fizikia.

Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Blasius Chatanda, alithibitisha kushikiliwa kwa mtuhumiwa huyo kwa kumshambulia mwanafunzi huyo Julai 3, mwaka huu, majira ya saa nane mchana.

Kwa mujibu wa Chatanda, mwanafunzi huyo akiwa darasani na wanafunzi wenzake, mtuhumiwa alitaka asome somo hilo baada ya kubaini ana uwezo nalo.

Alisema baada ya mwanafunzi huyo kukataa, inadaiwa mtuhumiwa alianza kumshambulia kwa kumchapa viboko sehemu mbalimbali za mwili na kusababisha kulazwa Kituo cha Afya Kimeya.

"Mtuhumiwa alimtaka alisome somo hilo kwamba ni somo lenye kipaumbele katika shule hiyo na baada ya kukataliwa alishindwa kuzuia hasira zake ndipo alitoa adhabu ya viboko vyenye kupitiliza, " alisema na kuongeza:" adhabu hiyo yenye kupitiliza kwa mwanafunzi huyo ililazimu kumkimbiza kituoni kupatiwa huduma ya kwanza."

Alisema jeshi hilo linaendelea na uchunguzi kwa hatua zaidi za kisheria.


bgtl

**BEST GROUP (T) LIMITED**

**Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant**

## MNADA WA HADHARA(MARUDIO)

**Best Group (T) Limited** kwa idhini tuliyopewa na **Bulyahulu Gold Mine Limited** tutauza kwa mnada wa hadhara baadhi ya vifaa, mitambo na mashine chakavu siku ya Jumamosi tarehe 20/07/2024 kunzia Saa 4.00 Asubuhi na kuendelea hapo hapo **Bulyanhulu Gold Mine:-**

**VITU VITAVYOUZWA**

**LOADER SKID STEER CAT236B, EXCAVATOR CAT325BL, TRACK DOZER CATD8R, FORKLIFT; MANITOU MVT665T_6.5T, FORKLIFT MANITOU 8T, CATERPILLAR DP30N FORKLIFT 3T, TRUCK TATA 713 S _LPK, HAULAGE TRUCK VOLVO, HAULAGE TRUCK TH540, TRUCK TH430 SANDVIK, DRILL QUASAR FACE DD210, INTEGRATED TOOL CARRIER CAT, HEAVY MOBILE LOADER, LOADER TORO T151D, LH307 SANDVIK, DRILL LONGHOLE DL311-7, LOADER 7 YARD, TRACTOR MASSEY FERGUSON, ATLAS COP SIMBA1257 PRODUCTION, FLAT BED TRUCK BOART SECO, HAULAGE TRUCK CAT730**

**MASHARTI YA MNADA**

1. Washiriki wote wa mnada lazima kufuata na kuzingatia masharti ya afya, mazingira na usalama waingiapo mgodini ikiwa ni pamoja na kuwa na vifaa vyote muhimu vya usalama mfano viatu vigumu vya usalama, kofia ngumu na nguo zenye viakisi.
2. Washiriki wanaruhusiwa kuingia kukagua vitu vinavyouzwa kuanzia tarehe 17/07/2024 hadi 19/07/2024 saa 4.00 asubuhi hadi saa 10.00 jioni.
3. Wanunuzi wote watalipa kodi zote ambazo vifaa vinavyouzwa vilisamehewa kodi hapo awali.
4. Kila mshiriki atatakiwa kulipa kiingilio cha kushiriki kiasi cha Tsh 10,000,000/= ilikupewa kadi maalumu ya kushiriki mnada, , iwapo mteja hatanunua kitu chochote kiasi chote alicholipa kwa ajili ya kiingilio kitarudishwa kwenye akaunti ya Benki ya mteja ndani ya siku saba (7) za kazi baada ya mnada.
5. Malipo kwa ajili ya kiingilio yalipwe kwenye akaunti

**Account- 22310047571 (TSHS)**
**Jina la Account-BEST GROUP (T) LIMITED**
**Jina la Benki- NMB Bank PLC**

6. Malipo mengine nje ya kiingilio yatalipwa kwenye akaunti

**Account 0106092142500 (TSHS)**
**Jina la Account-BULYANHULU GOLD MINE LTD**
**Jina la Benk- Standard Chartered**

7. Mnunuzi atatakiwa kulipa asilimia 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada na iwapo hatafanya hivyo bidhaa aliyonunua itauzwa kwa wateja wengine
8. Malipo yaliyobakia ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku 3 za kazi, kushindwa kufanya hivyo kutapelekea kupoteza malipo yote ya awali yaliyotolewa na bidhaa husika kuuzwa kwa wateja wengine.
9. Kila kitu kinauzwa kama kilivyo na hali yake na muuzaji hawajibika kwa namna yoyote ile kwa hali ya bidhaa inayouzwa .
10. Bidhaa zote zilizonunuliwa zinatakiwa zitolewe mgodini ndani ya siku 14 za kazi, na iwapo mteja hatatoa kwa wakati huo aliopewa atalipa gharama za ziada kwa ajili ya kuacha mali yake mgodini ndani kwa siku za kazi 16 zingine, baada ya hapo mgodi utauza mali zako kwa wateja wengine.
11. Hakuna bidhaa itakayotolewa bila kuwepo kwa idhini ya kuchukua bidhaa kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)
12. Kila mteja anapokuja kuchukua bidhaa zake atatoa taarifa ya siku moja kabla, na atalazimika kuwa uthibitisho wote wamalipo, nyaraka za manunuzi na barua kutoka TRA yakuwa amelipa kodi zote kuhusiana na bidhaa yake na vitambulisho vinavyomtambulisha kwa mujibu wa Sheria iwapo sio mnunuzi mwenyewe awe na mamlaka ya kisheria yanayompa uhalali kufanya hivyo
13. Wateja wote wanashauriwa kuzingatia taratibu za nchi katika ulipaji wa kodi, usafirishaji wa mizingo kwa kuwa na vibali vyote muhimu kuepuka usufumbu, pia watumie mawakala waliosajiliwa kwa mujibu wa sheria kuepuka usumbufu.
14. Muuzaji anaweza kuahirisha mnada muda wote wote iwapo kutakuwa na haja ya kufanya hivyo au kuondoa bidhaa yoyote katika orodha ya vitu anavyouza kabla ya kuuza kwa mteja.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na**
**Best Group (T) LTD**
**P O BOX 1088 DAR ES SALAAM**
**info@bestgroup.co.tz**
**+255715363537/+255765 363537**

DARASA CHINI YA MTI

# Walimu wadaiwa kupiga mwandishi

**Na Romana Mallya**

MHARIRI wa Habari za Biashara wa gazeti The Guardian na Mkuu wa Nipashe Digital, Dickson Ng'hily, amedai kushambuliwa na kupigwa na walimu wa Shule ya Msingi Kwembe, wilayani Ubungo, Dar es Salaam.

Tukio hilo amedai lilitokea jana asubuhi baada ya kupiga picha wanafunzi waliokuwa wanafundishwa na walimu wakiwa wameketi chini ya mti shuleni huko.

Ng'ily amedai kuwa baada ya kupiga picha hizo, mwanamume, ambaye baadaye alibaini ni Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, alimfuata, akihoji sababu za kupiga picha shuleni.

Katika mazungumzo na mwandishi wa habari hii baada ya kuachiwa kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ubungo alikopelekwa baada ya kukamatwa shuleni, Ng'ily alisema:

"Ilikuwa kati ya saa tatu na saa nne asubuhi wakati nikitoka nyumbani kwenda kazini. Ninaishi jirani na shule hii. Nilikuta wanafunzi wakiwa katika makundi mawili wamekaa chini, walimu wakiendelea kuwafundisha na imekuwa ikifanyika hivyo.

"Nikaona nipige picha kwa ajili ya matumizi ya kihabari. Wakati ninaendelea na zoezi hilo, nilisikia mmoja wa walimu akimwambia mwenzake 'mgeni wako anapiga picha'.

"Yule mwalimu akaja, sikujua nafasi yake, lakini baadaye nikajua ni Mwalimu Mkuu shuleni hapo. Akaniuliza 'kwanini unapiga picha?', nikamwambia, 'ninapiga picha watoto wamekaa juani wanasoma'. Akaniuliza 'kwani hapo ni juani?' nikamwambia 'hapo ni nje'."

"Akaniambia 'unajua tumekubaliana nini mpaka iwe hivyo?' Nikamwambia ninapiga kwa ajili ya habari.

"Akaniambia 'futa picha na kunihoji kama nina kibali', nikamjulisha 'sina na nimepiga nikiwa barabarani'.

Ndipo aliponiambia 'huwezi kupiga picha shuleni bila kuwa na kibali', nikamwambia 'hakuna tangazo lolote linaloonesha kukataza kupiga picha na kama lingekuwapo ningeliheshimu', alisema.

Ng'ily alidai kuwa baada ya mahojiano hayo, ndipo wakaibuka walimu wenzake na mmoja wao (mwanamke) akaamuru anyanganywe simu na vurugu zikaanza ikiwamo kupigwa fimbo mgongoni na kuangushwa chini.

"Mwalimu Mkuu akaona wataniumiza zaidi, akawakataza ndipo walipoacha, nikaomba wanipeleke sehemu salama, walinipeleka kwa Mtendaji wa Mtaa wa Kwembe; naye aliniomba kibali na nilivyojieleza, waliniomba kitambulisho cha kazi, nikawapa na simu walininyang'anya ikiwa imepasuka kioo," alidai.

Alisema kuwa hadi saa saba mchana, aliendelea kubaki ofisini kwa mtendaji huyo na baadaye akapelekwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ubungo. Taarifa zilikuwa zimeshaenea maeneo mbalimbali kuhusu kilichomsibu. Baadaye akaachiwa kwa agizo la Mkuu wa Wilaya, Hassan Bomboko ambaye hakuwa ofisini wakati anafikishwa huko.


Alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia suala hilo, Mkuu wa Wilaya Bomboko alisema: "Nilikuwapo ofisini kwangu hadi saa 6:15 mchana (jana), huyo mwandishi wa habari sikumwona akiletwa kwangu hadi nilipoondoka kuja Mburahati.

"Kama kuna jambo hilo, ninampigia simu sasa hivi Katibu Tawala wamwachie huyo mwandishi, ingawa naye amekwenda kinyume cha maadili ya taaluma yake kwenda shuleni kupiga picha pasipo kutoa taarifa kwa uongozi. Mwambieni awe anafuata taratibu sahihi, ili kuepuka mambo kama haya."

Kwa mujibu wa Ng'illy, aliachiwa huru baada ya Mkuu wa Wilaya Bomboko kumpigia simu Katibu Tawala majira ya alasiri.

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) ulitoa taarifa kwa umma jana, ukilaani kitendo cha walimu kushambulia na kupiga mwandishi wa habari.

"THRDC inaamini kwamba mwandishi wa habari ana haki ya kutafuta na kusambaza habari kwa umma kwa mujibu wa Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kupiga picha ni jambo la kawaida," ilisema taarifa ya mtandao huo.





Picha zinazodaiwa kusababisha Mwandishi wa Habari, Dickson Ng'hily ashambuliwe na walimu wa Shule ya Msingi Kwembe, Ubungo, Dar es Salaam jana.

# Mfanyabiashara mwenye deni kutopata nafasi soko Kariakoo

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, ametangaza utaratibu wa wafanyabiashara kuingia Soko Kuu la Kariakoo, linaloendelea kujengwa jijini Dar es Salaam na kuwataka wenye madeni kuyalipa kwanza.

Chalamila alitoa kauli hiyo juzi katika mkutano wa hadhara ikiwa ni mwendelezo wa ziara ya siku saba ya Katibu wa NEC, Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM Taifa, Amos Makalla, anayoifanya mkoani humo.

Akisimamia mchakato wa kujibu kero za wananchi zilizotolewa katika mkutano huo, Chalamila alimweleza Makalla kwamba, masoko mengi ya mkoa huo hayafanyi kazi vizuri kwa sababu ya kuvamiwa na madalali.

Aidha, hayaingizi fedha za kutosha kwa kuwapo baadhi ya watu waliojenga vibanda katika maeneo ya serikali na kusababisha migomo ya kutokulipa na sasa mkoa umeweka mkakati mzuri wa kutibu tatizo hilo.

Kuhusu Soko Kuu la Kariakoo, Chalamila alisema kwa sasa ujenzi umefikia asilimia 96 na litakapokamilika wataingia wa zamani na wapya watakaohitaji.

"Lakini soko lile zamani (Kariakoo) kulikuwa na watu wanakaa pale ambao hawakulipa madeni na kwa mantiki hiyo litakapofunguliwa na Rais (Samia Suluhu Hassan), wote waliokuwapo mheshimiwa mgeni rasmi, sheria ya kwanza watatakiwa kulipa madeni yote waliyokuwa nayo awali.

"Kwa sababu soko lilipoungua halikuchukua madeni hayo. Cha kwanza lazima ulipe madeni yote, cha pili lazima kutia saini mkataba ndipo uingie," alisema.

Chalamila alisema kama kutakuwa na mtu anayerembaremba watatoa siku tatu au nne ili wengine wajue siri ya kufanya biashara Kariakoo.

"Tumesema ule utaratibu wa kuingiza watu 'washamba washamba' katika masoko makubwa ya kimataifa haupo, huo muda umepitwa na wakati, Sh. bilioni 28 zilizowekwa halafu tuweke watu wa kuanza kulegalega na kupoteza taswira ya Mkoa wa Dar es Salaam, labda sipo Mkoa wa Dar es Salaam," alisisitiza.

Chalamila alisema lazima wafanye siasa na kukuza uchumi kwa kuwa mtu hawezi kuongea ongea akiwa na njaa.

"Tunaweka siasa kando tunatengeneza uchumi, hii ndio njia ya kwenda kwenye uponyaji. Na masoko nimewaambia, Mkurugenzi wa Jiji upo hapa, zamani tulikuwa na wasanifu majengo hawa watu sijui walizaliwa nchi gani.

"Anachora soko lina ghorofa karibu tatu halafu machinga (wafanyabiashara wadogo) wauzie juu na wenye mitaji mikubwa wauzie chini. Kinachotokea chini bei rahisi halafu juu ghali. Haiwezekani mtu apandishe juu kwa machinga kununua bidhaa, tumebadilisha ujenzi wa masoko," alisema.

Akizungumza katika mkutano huo wa hadhara, Makalla alimweleza Mkuu wa mkoa huo kwamba, alipoziona kero zilizotolewa na wananchi (zikiwamo zilizojibiwa) alifahamu zote zipo ndani ya uwezo wake.

"Kikubwa ninakuachia hiyo karatasi na huo mkeka kila mtu na namba yake, anatoka wapi na aina ya kero na utatuzi wake, nina amini baada ya kumaliza ziara hii utajipa muda wa wakurugenzi, watendaji wako ili mpate majibu na wananchi waridhike na majibu yenu," alisema.

Hivi karibuni, Rais Samia wakati akiwaapisha wateule aliowateua, alimwagiza Waziri mpya wa Viwanda na Biashara, Selemani Jafo, kuhakikisha kuwa biashara katika Soko la Kariakoo zinafanyika saa 24 ujenzi utakapokamilika.

Alimwagiza pia, kufanya kazi kwa ukaribu na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wizara ya Mipango na Uwekezaji pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ili kusimamia sekta ya biashara katika soko hilo na kuhakikisha kunakuwa na uhusiano mzuri baina ya wafanyabiashara na serikali nchini pamoja na kutatua kero zao.

Julai 10, mwaka 2021, Soko Kuu la Kariakoo liliungua moto, huku wafanyabiashara 224 wakipoteza bidhaa zao na serikali kutangaza kufanyia ukarabati pamoja na kujenga jengo jipya la ghorofa nne juu na mbili chini.

Soko hilo linajengwa na Kampuni ya Estim Construction na litakapokamilika litakuwa na uwezo wa kuchukua wafanyabiashara 2,300 sawa na ongezeko la 638 ikilinganishwa na 1,662 waliokuwapo kabla ya ukarabati wa jengo la zamani na ujenzi wa jengo jipya.

Kero nyingine zilizotolewa zilihusisha changamoto ya majitaka yanayotitirika mtaani, tatizo la umeme na nyingine zikihusisha mtu binafsi ambazo mkuu wa mkoa huo aliahidi kwenda kuzifanyia kazi pamoja na timu yake.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Wauza vipodozi muwe mnajali afya za wateja wenu

**WAFANYABIASHARA** wa vipodozi wanajukumu kubwa kuhakikisha wateja wao wanakuwa salama kwa kutumia bidhaa wanaouza bila kupata madhara.

Lakini baadhi yao wamekuwa wakiingiza vipodozi vyenye viambata vya sumu na kusababisha watu kuharibika ngozi na hatimaye kupata magonjwa ya saratani.

Pamoja na serikali kupiga marufuku uingizaji wa bidhaa za vipodozi vyenye viambata vya sumu, lakini baadhi ya wafanyabiashara hao hutumia njia za panya kuziingiza nchini.

Hata uuzaji wake huwa ni wa siri na wanaowauzia ni wateja wao waliowazoea.

Kuna maduka katika baadhi ya sehemu hufunguliwa nyakati za usiku pekee ili kuuza vipodozi hivyo na wateja wao wanayajua yalipo.

Hii ni hatari kwa sababu wananchi wanaendelea kuathirika kwa kukosa uelewa wa kutumia bidhaa hizo zilizopigwa marufuku.

Katika kukabiliana na suala hilo, Shirika la Viwango Nchini (TBS), limewataka watu wote wanaofanyabiashara ya chakula na vipodozi kusajili maeneo yao ili iwe rahisi kukaguliwa kwa ajili ya usalama wa afya za wananchi.

Vile vile, shirika limewataka wafanyabiashara na watumiaji wa bidhaa kuhakikisha bidhaa wanazonunua zina nembo ya alama ya ubora.

TBS imesisitiza kuwa wanaofanyabiashara ya vipodozi wanapaswa kuhakikisha vipodozi hivyo havina viambata sumu vyenye madhara kwa afya za watumiaji.

Watumiaji wa vipodozi hivyo mara nyingi hupenda kubadili ngozi zao na kutaka kufanana na watu weupe bila kujua athari zake.

Wengi wanaotumia baadaye ngozi zao hupata madhara kiasi cha kushindwa kutembea kwenye jua kwa sababu ngozi zao zinakuwa zimeshaathirika.

Wengine hulazimika kutembea na miamvuli kujikinga na jua lisipenye moja kwa moja kwenye ngozi zao.

Madhara ya vipodozi hivyo pia ni ngozi kuungua na badala ya kupata rangi wanayoitaka huwa wekundu na hatimaye weusi kama rangi ya mkaa.

Pamoja na elimu ya kuwataka wananchi kuacha kutumia vipodozi vyenye viambata vya sumu, lakini ni kama inawashawishi kuendelea kutumia kwa kutaka kubadili ngozi waliyozaliwa nayo na kuiga rangi za watu weupe.

Mara kwa mara tumeshuhudia TBS ikiteketeza tani kwa tani za vipodozi vyenye viambata vya sumu, lakini wafanyabiashara wanaendelea kuviingiza na kuangamiza maisha ya wananchi wenzao.

Na kwa wanaotumia bidhaa hizo wakumbuke kuwa urembo sio mtu kuwa mweupe, hata hao wenye rangi nyeupe wanatamani wawe weusi, lakini wanashindwa wataipataje.

Ndio maana hao wanaoonekana kuwa warembo kwasababu ya rangi zao nyeupe, wanajianika kwenye jua ili wapate rangi nyeusi.

Ni lazima kabla ya kuiga kitu mtu afahamu faida na hasara zake kabla ya kuamua kukifanya.

TBS ina kazi kubwa ya kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maduka yanayouza vipodozi ili kuwabaini wanaoendelea kuviingiza.

Na wenye viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo pia wanapaswa kukaguliwa ili kujiridhisha wanazalishwa kwa ubora unaotakiwa.

Kuthibitisha ubora wa bidhaa wanazozalisha na mifumo ya kimenejimenti na kusajili bidhaa za chakula na vipodozi.

Wanunuzi wa bidhaa hizo pia wanatakiwa kuthibitisha kuwa zina nembo ya uhakiki wa TBS ili kuwa na uhakika kwamba ni yenye ubora na ikitumiwa haileti madhara kwa mtumiaji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

## Tusifanye masihara tukazembea kula mboga, matunda kuna haya...

**KITENDO** cha jamii kupuuza ushauri wa wataalamu wa afya, chakula na lishe wa kuzingatia ulaji wa mboga katika mlo kila siku, si sahihi, kataeni ndio inaimarisha mwili wako, hata kupambana na magonjwa.

Pamoja na Tanzania kujaliwa kuwa na ardhi inayostawisha mazao mbalimbali, inaelezwa kuwa ulaji wa mboga unaojumuisha jozi ya matunda, bado mwitikio ni mdogo katika jamii.

Kwa mantiki hiyo, jamii inapaswa kuelewa kuwa mboga zina umuhimu mkubwa katika mwili mwa binadamu.

Hata wataalamu wa afya na lishe ndani na nje ya nchi, wamekuwa wakihimiza jamii kula mboga na matunda, kama njia ya kupambana na magonjwa yanayotokana na upungufu wa kinga mwilini.

Shirika la Afya Duniani (WHO), linapendekeza mtu kula angalau gramu 50 za mboga kwa siku, lengo kufikisha kilo 80 kwa mwaka.

Shirika hilo linataka hamasa jamii ihamasishwe kuhusu umuhimu wa mboga mboga kwenye lishe kama njia ya kujenga afya bora kwa jamii.

Utafiti tofauti, umebaini walaji mboga wengi hawali nyama, kuku, samaki na bidhaa kutoka kwa wanyama, ikiwa ni pamoja na mayai na maziwa.

Imebainika kuwa watu wengine hawali mboga na matunda kwa sababu hawafahamu faida zake kwa kwa afya zao.

Wapo wanaoamini kula mboga kunatokana na ushauri wa daktari kwa mgonjwa, ili kukabiliana na hali ya maradhi yake na kuongeza kiwango cha chembe hai mwilini.

Wengine wanaamni kuwa ni vigumu kula mboga bila nyama, kuku na samaki.

Watafiti wamegundua kuwa mtu asiyekula nyama, kuna uwezakano mdogo wa kupatwa na maradhi ya moyo na saratani.

Kwa njia nyingine, ni kuwa mtu asiyekula nyama alihusishwa na afya nzuri, japokuwa ana uwezekano wa kuishi miaka mingi duniani.

Kulingana na Taasisi ya Chakula na Lishe nchini, ulaji mboga na matunda katika jamii uko chini, kwa sababu idadi kubwa ya watu hawapendi kutumia vyakula hivyo.

Siku hiyo ya uadhimishwa kila mwaka, kwa lengo la kuhamasisha ulaji vyakula, hivyo ili jamii ikabiliane na magonjwa yasiyoambukiza, ikiwamo hali ya unene uliopitiliza.

Siku hiyo inaadhimishwa wakati kilimo cha mboga na matunda kimehamasishwa duniani kwa miongo mingi na hata nchini kimeshamiri.

Kwa mujibu wa taasisi hiyo, takwimu za ulaji matunda na mboga, ni changamoto kwa sababu watu hawapendi kula vyakula hivyo kwa kisingizio kuwa ni gharama.

Hata hivyo, inahimiza jamii kula matunda na mboga zilizopo kwenye msimu ambayo huuzwa kwa bei ya chini.

Mboga na matunda yana vitamini na madini yanayosaidia mwili kukingwa na magonjwa, yakiwamo ya mfumo wa hewa kama mafua ambao uchochewa na ukosefu wa matunda na mboga mwilini, hivyo ulaji wake unasaidia kupandisha kinga ya mwili na kutoweka.

Magonjwa yanayosababishwa na ukosefu wa Vitamini C mwilini ni kutokwa na damu kwenye fizi, meno kung'oka, ngozi kavu, wekundu kwenye vinyweleo, kuchubuka, kuvimba viungo.

Ukosefu wa Vitamini A, unasababisha ukavu katika ngozi, kupata vidonda kwenye ngozi, uoni hafifu na macho kuwasha.

Vyakula vingine vyenye Vitamin A ni maboga, viazi vitamu hasa vya njano, mboga za kijani sana, mahindi ya njano, siagi, samaki, kiini cha yai, figo za wanyama na matunda ya njano ya papai, karoti na maembe.

Magonjwa yanayosababishwa na ukosefu wa Vitamini K ni damu kutoganda.

Wataalamu wanashauri ulaji mbogamboga na matunda yenye rangi tofauti wa rangi kwa ajili ya vitamin matunda machachu ya ukwaju, chungwa na limao yana vitamini nyingi.

Tofauti ya rangi ndivyo zinavyotofautiana kwenye vitamini, wataalamu wakishauri ulaji boga au tunda hilo hilo kila siku.

Matunda machachu kama ukwaju, chungwa, limao yanatajwa kuwa na vitamini kwa wingi.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO), linasema usalama wa chakula ni muhimu na inaonya kisicho salama ni hatari kwa maisha ya binadamu.

Takwimu za FAO zinaonyesha kila mwaka watu 600,000 huugua kutokana na kula chakula kisicho salama, kati yao hao 420,000 hufa.

FAO inafafanua kuwa mtu mmoja kati ya 10 hufa kila mwaka kwa kula chakula kisicho salama kutokana na kuwa na vimelea, bakteria, virusi, kemikali na wadudu.

## Ustawi wa Jamii waanzisha mtaala mpya malezi, makuzi

**Na Pilly Kigome**

CHUO cha Ustawi wa Jamii kimetangaza kuanza udahili wa mtaala mpya wa malezi na makuzi ya awali ya mtoto ili kuleta tija katika jamii pamoja na kukabiliana na ukatili dhidi ya watoto.

Ofisa Uhusiano wa chuo hicho, Benedict Nkwao, kwa niaba ya Mkuu wa Chuo, Dk. Joyce Nyoni, alitangaza hatua hiyo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari katika Maonesho ya 48 ya Sabasaba jijini Dar es Salaam.

Alisema mtaala huo mpya mahususi unakwenda kusuka wakufunzi na wataalamu wa kwenda kufundisha walimu wa watoto, walezi wa watoto, ikiwamo kwenye vituo vya kulea watoto na vituo vya 'daycare' na makundi mengine yahusuyo watoto.

Nkwao alisema mtaala huo utatolewa kwa ngazi ya Cheti na Diploma katika Kampasi ya Kisangara Mwanga mkoani Kilimanjaro.

Aidha, alifafanua kozi hiyo itakwenda kutoa suluhisho kusaidia kuwajenga kuhusu malezi ya watoto kwa kuwa jamii inakabiliwa na changamoto kubwa katika malezi hayo ikiwamo ukatili kwa watoto.

Mtaala huo utakwenda kuwaongoza katika ulinzi wa mtoto, kuwafundisha taratibu za kuwaongoza katika michezo ya watoto, saikolojia ya mtoto, sanaa na vingine vingi vinavyohusu makuzi ya mtoto kwa ujumla.

Alifafanua tayari chuo kimeshaanza kudahili wanafunzi hivyo kuwataka Watanzania kuchangamkia fursa hiyo, ili waweze kwenda kujiunga na kozi hiyo muhimu katika ustawi wa mtoto.

"Watanzania wanafunzi wenye uhitaji kutaka kujiunga kozi hii waje wajitokeze kwenye banda letu hapa hapa tunafanya usajili."

Wakazi wa jijini Dar es Salaam waliyoongea na Nipashe walisema kuwa chuo hicho kimeona mbali kwa kuleta kozi hiyo mpya ambayo itakwenda kukomboa watoto shuleni na katika vituo vya watoto.

"Walezi watakuwa wamesukwa vya kutosha kuhusiana na malezi ya mtoto kwa ujumla," alisema Anna Rahael.

**Alisema mtaala huo mpya mahususi unakwenda kusuka wakufunzi na wataalamu wa kwenda kufundisha walimu wa watoto, walezi wa watoto, ikiwamo kwenye vituo vya kulea watoto na vituo vya 'daycare' na makundi mengine yahusuyo watoto.**

# DCI awahakikishia wananchi usalama

**Na Maulid Mmbaga**

MKURUGENZI wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Kamishna Ramadhani Kingai, amesema nchi kwa sasa iko salama kutokana na utendaji kazi wa maofisa wa Jeshi la Polisi ambao wanasimamia haki katika kutimiza jukumu lao kubwa la kuzuia uhalifu.

Aliyasema hayo juzi mkoani Dar es Salaam, wakati wa hafla ya kuwatunukia vyeti maofisa 13 wa Jeshi la Polisi kama ishara ya kutambua mchango wao wa kujituma kwa bidii kazini kwa kuzingatia haki na sheria.

"Tunao utaratibu wetu ndani ya jeshi kwamba askari wanaofanya vizuri zaidi kushinda wenzao na kuonyesha mfano mzuri wa utendaji ndani ya Jeshi la Polisi kwa kufuata sheria, taratibu, kanuni, nidhamu, haki na weledi tunawazawadia ili kuwaongezea ari ya utendaji kazi," alisema DCI Kingai.

Aidha, aliongeza kuwa kufanya hivyo ni kutoa chachu kwa askari wengine kuendelea kufanya kazi kwa kuzingatia miongozo ya kimaadili ya kazi ili kuimarisha utendaji wa Jeshi la Polisi nchini.

Ofisa wa Operesheni Mageni Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Denis Simbeye, ambaye ni miongoni mwa waliotunukiwa cheti hicho, alisema zawadi walizopewa itakuwa chachu na itawapa morali na kuongeza bidii zaidi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Pia alisema kazi yao kubwa ni kuhakikisha wananchi wanaishi kwa amani bila bugudha kutoka kwa wahalifu mbalimbali na kwamba kilichofanyika kitawapa hamasa watu wengine wanaoshirikiana nao kuhakikisha wanaendelea kupambana na uhalifu.

"Tunamshukuru mkuu wa jeshi letu la polisi kwa kutunuku vyeti hivi kutokana na utendaji kazi tulioufanya kwa kipindi cha mwaka 2023/24, zawadi hizi tumepokea kwa niaba ya wenzetu wote tunaoshirikiana nao katika kazi tunayofanya ya kupambana na wahalifu na uhalifu.

"Tunafanya yote haya kwa kuzingatia maelekezo tuliyopatiwa ikiwamo na Tume ya Haki Jinai, kwa kuzingatia sheria, kwa hiyo hii kwetu ni chachu kubwa na tunaahidi kupitia hii wananchi wategemee kupata huduma bora zaidi katika kuhakikisha tunalinda usalama wao na mali zao," alisema Simbeye.



Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024, Godfrey Mnzava, akipanda mti kwenye ujenzi wa mradi wa mabwawa ya kutibu majitaka unaojengwa eneo la Manga, Kata ya Mtipa, Manispaa ya Singida jana. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# TET, Educate kumaliza uhaba walimu

**Na Maulid Mmbaga**

TAASISI ya Elimu Tanzania (TET), imeanzisha programu ya kuajiri walimu wa kujitolea kwa somo la biashara katika shule zitakazoainishwa kuwa na uhitaji mkubwa lengo likiwa ni kukabiliana na uhaba wa walimu.

Mkurugenzi wa TET, Dk. Aneth Komba, alisema hayo wakati wa hafla ya kutia saini makubaliano ya ushirikiano kati ya taasisi hiyo na Shirika lisilo la kiserikali la Educate.

Alisema programu hiyo ni sehemu ya makubaliano hayo ambayo yatasaidia pia kuajiri walimu kwa mkataba katika shule zenye uhitaji.

Kwa mujibu wa Dk. Aneth, makubaliano hayo yanalenga pia kuwezesha TET kuwa kitivo cha utafiti utakaosaidia kukuza na kubadilishana uzoefu na ujuzi katika utekelezaji wa mafunzo ya somo la biashara, pamoja na kumuandaa mtanzania anaeweza kushindana kimataifa.

"Mkataba huu unalenga pia kushirikiana kwenye kuimarisha utoaji wa mafunzo endelevu kwa walimu shuleni hasa katika somo la biashara na kuwawezesha kufundisha somo hilo kwa kutumia mbinu za kisasa na kuwa na maarifa yanayoendana na wakati katika ufundishaji.

"Niwaombe walimu ngazi ya sekondari watengeneze jumuia za ujifunzaji na wajifunze kupitia matini mbalimbali ambayo yako kwenye mfumo wa 'learning management system' ambao unapatikana bure," alisema Dk. Aneth.

Aidha, alibainisha kuwa mtaala mpya ulioboreshwa umeanza utekelezaji wake rasmi mwezi huu kwa kidato cha tano na elimu ya ualimu stashahada, na kwamba TET imejipanga vizuri kuhakikisha maandalizi ya kutoa mafunzo kwa walimu pamoja na vifaa vya ufundishaji vinakuwapo.

Pia, alisema mtaala ulioboreshwa ambao unatekelezwa kwa sasa unatokana na sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014 toleo la 2023, ambalo linasisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya serikali, sekta binafsi na wadau mbalimbali wa maendeleo kutoa elimu bora kwa ngazi zote nchini.

"Educate wamekuja wakati mwafaka wakati tunaendelea na utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa, ambayo jambo kubwa ni kuanzishwa kwa somo jipya la biashara ambalo ni la lazima ngazi zote za elimu," alisema Dk. Aneth.

Alisema kuwa uanzishwaji wa somo la biashara unatokana na maoni ya wadau kwa takribani asilimia 93 ambao waliyakusanya na katika utekelezaji wake walitia saini makubaliano na Educate kwa kipindi cha mwaka mmoja ambayo yaliisha mwaka huu, na jana kusaini mapya.

Aidha, alisema katika ushirikiano wa awali walipata matokeo chanya ikiwamo kupata fursa ya kutembelea Rwanda kwaajili ya kujifunza na kubadilishana uzoefu na kwamba kutokana na mafunzo hayo wameandaa muktasari wa somo la elimu ya biashara, kitabu na kiongozo cha mwalimu.

Mengine ni miongozo ya kuendesha klabu za somo la biashara kwa wanafunzi, pamoja na mafunzo kwa walimu, na kufanya utafiti ndogo.

Mkurugenzi wa Shirika la Educate, Kamanda Kamiri, alisema tangu 2022 katika awamu ya kwanza ya ushirikiano walipata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa mtaala, na kwasasa wametia saini makubaliano pia ili kuendeleza walipoishia.

"Lengo letu ni kuhakikisha kwamba tunawandaa watoto kukabiliana na maisha baada ya kuhitimu, kwa kuwapatia maudhui mazuri yanayoendana na dunia ya sasa, tumeshamaliza awamu ya kwanza sasa tuko katika awamu ya pili, ikiwamo kutoa elimu kwa walimu," alisema Kamiri.

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## SHINYANGA REGION
## PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
## KISHAPU DISTRICT COUNCIL

HALMASHAURI YA WILAYA KISHAPU

# FINANCIAL STATEMENT FOR THE FINANCIAL YEAR ENDED 30 JUNE 2023

## STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 30TH JUNE, 2023

| | Note | 2023 (TZS) | Restated 2022 (TZS) |
|---|---|---|---|
| ASSETS | | | |
| Current Asset | | | |
| Cash and Cash Equivalents | 62 | 2,964,610,936 | 1,470,786,720 |
| Receivables | 67 | 2,218,662,494 | 1,045,642,372 |
| Prepayments | 69 | 632,688,918 | 736,355,164 |
| Inventories | 70 | 1,250,600,771 | 984,369,237 |
| Other Financial Assets | 71 | 59,058,700 | 59,058,700 |
| Total Current Asset | | 7,125,621,819 | 4,296,212,194 |
| Non-Current Asset | | | |
| Property, Plant and Equipment | 77 | 33,498,900,866 | 23,133,653,382 |
| Biological Assets | 79 | 182,294,073 | - |
| Work In Progress | 82 | 1,907,553,465 | 2,909,048,012 |
| Total Non-Current Asset | | 35,588,748,404 | 26,042,701,394 |
| TOTAL ASSETS | | 42,714,370,223 | 30,338,913,588 |
| LIABILITIES | | | |
| Current Liabilities | | | |
| Payables and Accruals | 89 | 2,234,442,275 | 1,400,232,805 |
| Deferred Income | 93 | 1,841,427,307 | 1,108,116,259 |
| Deposits | 94 | 426,061,479 | 172,395,325 |
| Total Current Liabilities | | 4,501,931,061 | 2,680,744,389 |
| Non-Current Liabilities | | | |
| Other Borrowings by Government Entities | 102 | 1,842,037,413 | 1,007,069,503 |
| Total Non-Current Liabilities | | 1,842,037,413 | 1,007,069,503 |
| TOTAL LIABILITIES | | 6,343,968,473 | 3,687,813,892 |
| Net Assets | | 36,370,401,750 | 26,651,099,696 |
| NET ASSETS | | | |
| Other Reserves | | 59,058,700 | 59,058,700 |
| Accumulated Surpluses / Deficits | | 36,311,343,050 | 26,592,040,996 |
| TOTAL NET ASSETS | | 36,370,401,750 | 26,651,099,696 |

Emmanuel Johnson
Council Director
Date 22-03-2024

William L. Jijimya
Council Chairman
Date 22-03-2024

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
KISHAPU DISTRICT COUNCIL
P.O. BOX 1288,
SHINYANGA.

CHAIRPARSON KISHAPU DISTRICT C
P.O. BOX 1288
KISHAPU - SHINYANGA

## CASHFLOW STATEMENT AS AT 30th JUNE, 2023

| | Note | 2023 (TZS) | 2022 (TZS) |
|---|---|---|---|
| CASH FLOW FROM OPERATING ACTIVITIES | | | |
| RECEIPTS | | | |
| Subvention from other Government entities | 32 | 32,684,149,589 | 30,524,022,370 |
| Social Contributions (Revenue) | 20 | 558,681,952 | 716,608,942 |
| Revenue from Exchange Transactions | 17 | 112,571,355 | 49,775,321 |
| Other Revenue | 31 | 419,886,790 | 411,060,282 |
| Levies | 18 | 2,614,382,375 | 1,689,989,636 |
| Increase in Deposit | 61 | 253,666,154 | - |
| Fees, Fines, Penalties and Forfeits | 19 | 20,173,631 | 2,900,500 |
| External Assistance | 25 | 1,669,431,200 | 2,242,554,271 |
| Total Receipts | | 38,332,943,045 | 35,636,911,322 |
| PAYMENTS | | | |
| Wages, Salaries and Employee Benefits | 34 | 24,835,201,067 | 21,520,575,979 |
| Use of Goods and Service | 35 | 5,306,789,774 | 5,212,289,055 |
| Social Benefits | 43 | 2,239,662,164 | 1,776,970,315 |
| Other Transfers | 60 | 334,425,201 | 258,391,106 |
| Other Expenses | 52 | 194,068,767 | 30,898,291 |
| Maintenance Expenses | 36 | 339,923,678 | 265,288,283 |
| Decrease in Deposit | 61 | - | 5,494,994 |
| Total Payments | | 33,250,070,650 | 29,069,908,022 |
| NET CASH FLOW FROM OPERATING ACTIVITIES | | 5,082,872,396 | 6,567,003,299 |
| CASH FLOW FROM INVESTING ACTIVITIES | | | |
| Investing Activities | | | |
| Payment for Work in Progress | 106 | (1,521,948,075) | (402,301,868) |
| Advance Payment for Acquisition of Property Plant and Equipment | 103 | - | (92,346,916) |
| Acquisition of Property, Plant and Equipment | 77 | (2,719,773,941) | (6,158,943,942) |
| Acquisition of Biological Assets | 79 | (182,294,073) | - |
| Total Investing Activities | | (4,424,016,089) | (6,653,592,726) |
| NET CASH FLOW FROM INVESTING ACTIVITIES | | (4,424,016,089) | (6,653,592,726) |
| CASH FLOW FROM FINANCING ACTIVITIES | | | |
| Cash proceeds from other short or long-term borrowings | 96 | 834,967,910 | - |
| Total Financing Activities | | 834,967,910 | - |
| NET CASH FLOW FROM FINANCING ACTIVITIES | | 834,967,910 | - |
| Net Increase | | 1,493,824,216 | (86,589,427) |
| Cash and cash equivalent at beginning of period | | 1,470,786,720 | 1,557,376,147 |
| Cash and cash equivalent at end of period | | 2,964,610,936 | 1,470,786,720 |

Emmanuel Johnson
Council Director
Date 22-03-2024

William L. Jijimya
Council Chairman
Date 22-03-2024

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
KISHAPU DISTRICT COUNCIL
P.O. BOX 1288,
SHINYANGA.

CHAIRPARSON KISHAPU DISTRICT C
P.O. BOX 1288
KISHAPU - SHINYANGA

## STATEMENT OF FINANCIAL PERFORMANCE AS AT 30th JUNE, 2023

| | Note | 2023 (TZS) | Restated 2022 (TZS) |
|---|---|---|---|
| REVENUE | | | |
| Revenue Grants | 16 | 2,676,457,030 | - |
| Revenue from Exchange Transactions | 17 | 216,712,155 | 49,775,321 |
| Levies | 18 | 2,715,109,695 | 1,726,510,227 |
| Fees, Fines, Penalties and Forfeits | 19 | 20,173,631 | 2,900,500 |
| Social Contributions (Revenue) | 20 | 1,964,533,689 | 872,608,942 |
| External Assistance | 25 | 1,669,431,200 | 2,242,554,271 |
| Other Revenue | 31 | 3,413,008,670 | 411,060,282 |
| Subvention from other Government entities | 32 | 32,585,074,022 | 31,075,448,873 |
| Total Revenue | | 45,260,500,092 | 36,380,858,416 |
| TOTAL REVENUE | | 45,260,500,092 | 36,380,858,416 |
| EXPENSES AND TRANSFERS | | | |
| Expenses | | | |
| Wages, Salaries and Employee Benefits | 34 | 25,196,411,568 | 21,355,943,567 |
| Use of Goods and Service | 35 | 6,409,239,851 | 3,707,596,022 |
| Maintenance Expenses | 36 | 339,923,678 | 956,284,672 |
| Depreciation of Property, Plant and Equipment | 37 | 845,190,595 | 265,288,283 |
| Other Expenses | 52 | 194,068,767 | 30,898,291 |
| Social Benefits | 56 | 2,239,662,164 | 1,776,970,315 |
| Total Expenses | | 35,224,496,622 | 28,092,981,150 |
| Transfer | | | |
| Other Transfers | 60 | 316,701,415 | 297,574,922 |
| Total Transfer | | 316,701,415 | 297,574,922 |
| TOTAL EXPENSES AND TRANSFERS | | 35,541,198,037 | 28,390,556,072 |
| Surplus / Deficit | | 9,719,302,054 | 7,990,302,344 |

Emmanuel Johnson
Council Director
Date 22-03-2024

William L. Jijimya
Council Chairman
Date 22-03-2024

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
KISHAPU DISTRICT COUNCIL
P.O. BOX 1288,
SHINYANGA.

CHAIRPARSON KISHAPU DISTRICT C
P.O. BOX 1288
KISHAPU - SHINYANGA

## STATEMENT OF CHANGES IN NET ASSET FOR THE PERIOD ENDED 30th JUNE, 2023

| | Accum. Surplus/(Deficit) TZS | Other Reserve TZS | |
|---|---|---|---|
| Opening Balance as at 01 Jul 2022 | 26,592,040,996 | 59,058,700 | 26,65 |
| Surplus/ Deficit for the Year | 9,719,302,054 | - | 9,71 |
| Closing Balance as at 30 Jun 2023 | 36,311,343,050 | 59,058,700 | 36,37 |
| Opening Balance as at 01 Jul 2021 | 18,601,738,651 | 59,058,700 | 18,66 |
| Surplus/ Deficit for the Year | 7,990,302,344 | - | 7,99 |
| Closing Balance as at 30 Jun 2022 | 26,592,040,996 | 59,058,700 | 26,65 |

Emmanuel Johnson
Council Director
Date 22-03-2024

William L. Jijimya
Council Chairman
Date 22-03-202

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
KISHAPU DISTRICT COUNCIL
P.O. BOX 1288,
SHINYANGA.

CHAIRPARSON KISHAP
P.O. BOX
KISHAPU - SHI

## REPORT ON THE AUDIT OF FINANCIAL STSTEMENTS

**Unqualified Opinion**

I have audited the financial statements of Kishapu District Council, which comprise the statement of financial position as at 30 June 2023, the statement of financial performance, statement of changes in net assets, cash flow statement and the statement of comparison of budget and actual amounts for the year then ended, as well as the notes to the financial statements, including a summary of significant accounting policies.

In my opinion, the accompanying financial statements present fairly in all material respects, the financial position of Kishapu District council as at 30 June 2023, and its financial performance and its cash flows for the year then ended in accordance with International Public Sector Accounting Standards (IPSAS) Accrual basis of accounting and the manner required by the Local Government Finances Act, Cap. 290.

**Basis for Opinion**

I conducted my audit in accordance with the International Standards of Supreme Audit Institutions (ISSAIs). My responsibilities under those standards are further described in the section below entitled "Responsibilities of the Controller and Auditor General for the Audit of the Financial Statements". I am independent of Kishapu district Council in accordance with the International Ethics Standards Board for Accountants' Code of Ethics for Professional Accountants (IESBA Code) together with the National Board of Accountants and Auditors (NBAA) Code of Ethics, and I have fulfilled my other ethical responsibilities in accordance with these requirements.

I believe that the audit evidence I have obtained is sufficient and appropriate to provide a basis for my opinion.

**Key audit matters**

Key audit matters are those matters that, in my professional judgment, were of most significance in my audit of the financial statements of the current period. I have determined that there are no key audit matters to communicate in my report.

**Other Information**

Management is responsible for the other information. The other information comprises the Report by those charged with governance, Statement of Management Responsibility and

Declaration by the Head of Finance but does not include the financial statements and my audit report thereon which I obtained prior to the date of this auditor's report.

My opinion on the financial statements does not cover the other information, and I do not express any form of assurance conclusion thereon.

**REPORT ON COMPLIANCE WITH LEGISLATIONS**

**Compliance with the Public Procurement laws**

**Subject matter: Compliance audit on procurement of works, goods, and services**

I performed a compliance audit on the procurement of works, goods, and services of Kishapu District Council for the financial year 2022/23 as per the Public Procurement laws.

**Conclusion**

Based on the audit work performed, I state that, except for the matters described below, procurement of goods, works and services of Kishapu District Council is generally in compliance with the requirements of the Public Procurement laws.

(i) ***Procurements made without inviting competitive quotations TZS 100,000,000***
My review of procurement undertakings at Kishapu District Council found that, the Council paid TZS 100,000,000 to National Ranching Company Ltd for procurement of 40 breeding bulls (cows) for the Ecosystem based adaptation for rural resilience project without observing competitive bidding process contrary to requirement of Regulations 163 & 164 of the Public Procurement Regulations, 2013 as amended by Regulation 62(g) of the Public Procurement (Amendment) Regulations, 2016.

(ii) ***Procured items delivered and accepted before inspection TZS 31,743,178***
During the year audit I found that, procured items worth TZS 31,743,178 were delivered and accepted by the Council before being inspected contrary to requirement of Regulation 245 of the Public Procurement Regulations, 2013.

**Compliance with the Budget Act and other Budget Guidelines**

**Subject matter: Budget formulation and execution**

I performed a compliance audit on budget formulation and execution in the Kishapu District Council for the financial year 2022/23 as per the Budget Act and other Budget Guidelines.

**Conclusion**

Based on the audit work performed, I state that, except for the matter described below, Budget formulation and execution of Kishapu District Council is generally in compliance with the requirements of the Budget Act and other Budget Guidelines.

*Under allocation of funds to department of agriculture, livestock and fisheries TZS 63,017,873*

Paragraph XI to XIII of the Guidelines for the Preparation of Annual Plan and Budget for 2022/23 requires the Council to allocate 20% of its own source revenue collected to be spent in department of agriculture, livestock and fisheries.

Contrary to the requirement indicated above, my review of revenue management found that, during the year the Council collected TZS 1,071,133,057 from which TZS 214,226,611 which is 20% was supposed to be allocated for agriculture, livestock and fisheries. However, the Council allocated TZS 151,208,738 leaving balance of TZS 63,017,873 equivalent to 29% not allocated.

Charles E. Kichere
Controller and Auditor General,
Dodoma, United Republic of Tanzania.
March 2024



## FAO kukiwezesha kituo mabilioni

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

KITUO cha Kimataifa cha Utafiti wa Mboga na Uhifadhi wa Mbegu (World Veg) kilichopo Wilaya ya Arumeru mkoani hapa kinatarajia kupokea zaidi ya Sh. bilioni 1.7 kutoka Shirika la Chakula Duniani (FAO) kwa ajili ya kuiwezesha Benki ya Mbegu kufikia malengo yake nchini.

Juzi, Mkurugenzi Mkuu wa kituo hicho Ukanda wa Afrika, Dk. Gabriel Rugalema, alisema wanatarajia fedha hizo hizo ambazo ni sawa na Euro 600,000 zitawasaidia katika shughuli ya kuhifadhi mbegu za asili.

Akitoa taarifa kuhusu ujio wa fedha hizo kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, Dk. Rugalema alisema kuwa kwa sasa wanaendelea kuweka vinasaba katika benki hiyo.

"Tumeshafikia wakulima 504, wanafunzi 120 na watu wa nje zaidi ya 600 wamepata elimu ya masuala ya kilimo cha mboga, hivyo kituo hiki kina umuhimu mkubwa kuleta ustawi wa kilimo hapa nchini," alisema.

Hata hivyo, alisema ulaji wa mboga nchini bado ni mdogo kwa jamii ingawa zina umuhimu mkubwa kwenye mwili wa binadamu kuimarisha afya na kupambana na magonjwa.

"Shirika la Afya Duniani (WHO), lenyewe linapendekeza mtu kula angalau gramu 50 za mboga kwa siku ili kufikisha kilogramu 80 kwa mwaka, hivyo hamasa inatakiwa kutolewa kuhusu umuhimu wa mboga mboga kwenye lishe," alisisitiza Rugemalila

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mariam Mzuzuri, alisema kutokana na kazi nzuri inayofanywa na kituo hicho, watapeleka mapendekezo yao wizara husika ili yafanyiwe kazi.

"Kituo kimekuwa na eneo dogo na tumeambiwa walishatuma maombi ya kuongezewea eneo ili kujipanua na wafanye kazi zao kwa ufanisi, hilo tumelibeba na tutahakikisha linafanyiwa kazi kwa haraka," alisema Mariam.

Mjumbe wa Kamati hiyo na Mbunge wa Babati Mjini, Pauline Gekul, alisema kulingana na utafiti unaofanywa na kituo hicho, ni vyema ukafanyika utafiti wa udongo kwa kila mkoa kutambua mboga gani inastawi vizuri eneo hilo na kuisogeza kwa wananchi.

# Wanavijiji wachangishana 'buku buku' kujenga barabara

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAKAZI wa vijiji vya Makami Juu na Makami Chini Kata ya Kilema Kaskazini wilayani hapa, Mkoa wa Kilimanjaro, wamechanga fedha kuanzia Sh. 1,000 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara inayowaunganisha na barabara kuu.

Hatua hiyo imekuja kutokana na ubovu wa barabara hiyo kusababisha shughuli za kiuchumi kukwama na kuharibu mitaji yao kutokana na wafanyabiashara na wakulima kushindwa kutumia soko lao la mazao.

Mratibu wa mradi wa ujenzi huo wa barabara za vijiji hivyo, Wolter Nguma, akizungumza jana katika hafla ya utiaji sahihi mkataba wa ujenzi wa barabara hizo na makandarasi wa Kampuni ya Milioni Engineering General Supply iliyopewa zabuni hiyo alisema lengo ni

kuinua uchumi katika eneo lao na kurahisisha upatikanaji wa huduma za jamii na za msingi.

"Ukiangalia eneo letu hili kwa asilimia kubwa, tunahitaji sana barabara hizi ziwe na maboresho makubwa ili kuweza kuinua uchumi wa watu wetu hapa. Tumeanza sisi kama kikundi (Wana Makami), lakini tunaamini sasa kama serikali ikishirikiana na sisi, uwezekano wa kuwaondoa watu wetu wa maeneo haya katika umaskini upo," alisema na kuongeza kuwa: Ukiutizama ni kama wamesahaulika tu. Lakini kama wangepewa kipaumbele, naamini hali za vijana wa hapa zingeweza kubadilika kwa kujiajiri kwenye sekta za kilimo, ufugaji na utalii."

Mmoja wa wakazi wa Makami Chini, Mathias Mboya, alisema katika nyakati za mvua wakazi wa vijiji hivyo, wamekuwa wakishindwa kuzifikia huduma za afya katika Hospitali ya Misheni ya Kilema kutokana na ubovu wa barabara hiyo na gharama za usafiri kuwa kubwa, tofauti na kipato chao.

"Nimefurahishwa sana na huu umoja wa wana Makami, kuchangia kwa ajili ya kutengeneza hizi barabara zetu kwa sababu mara nyingi imekuwa ni adha kubwa, hasa kipindi cha mvua, na tunapokuwa na wagonjwa, hospitali tunayoitegemea kwa upande wetu ni Hospitali ya Misheni ya Kilema. Wakati wa mvua barabara hazipitiki, hata bodaboda kupita ni shida,"alieleza Mboya.

Baada ya kuingia makubaliano hayo ya ujenzi, Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, Prosper Munishi, alikishukuru kikundi hicho cha Wana Makami kwa kufikiria juu ya kuitengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe, badala ya kuendelea kusubiri miradi ya serikali.



Meneja wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Mhandisi Cleophace Maharangata (kulia), akitoa taarifa ya mradi wa maji wa Mizembwe na Potwe kwa wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM wilaya hiyo, walipotembelea kukagua miradi ya maji wilayani humo hivi karibuni. Kutoka kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Zainab Abdallah, Mwenyekiti wa CCM Wilaya, Laick Gugu na Katibu wa CCM Wilaya, Simon Leng'ese. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wanawake wahamasishwa kugombea serikali za mitaa

**Na Cynthia Mwilolezi,** KITETO

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara (CCM), Regina Ndege amewataka wanawake kujitokeza kugombea nafasi za uongozi kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji unaotarajia kufanyika mwaka huu.

Ndege alitoa rai hiyo juzi katika Kata ya Kibaya wilayani hapa wakati akizungumza na wanawake kupitia Baraza la Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wa Chama cha Mapinduzi (CCM).

Aliwataka wanawake wasibaki nyuma kwenye uchaguzi huo wa mitaa, vijiji na vitongoji bali wajitokeze kwa wingi kwa sababu wana uwezo mkubwa wa kuongoza.

"Wanawake tunapaswa kuaminiana, kujiandaa na kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa, kwa kuomba nafasi mbalimbali za uongozi," alisema Ndege.

Alisema wanawake wasijihisi wanyonge, kwani wanapaswa kufuata nyayo za Rais Samia Suluhu Hassan katika uongozi.

"Tusihofie chochote wanawake tuna uwezo mkubwa wa uongozi kwani hata nchi ipo mikononi mwa mwanamke na ipo salama na hapa Manyara tuna mwanamama mahiri mkuu wetu wa Mkoa Queen Sendiga," alisema.

Alisema anatarajia kwenye mkoa huo watajitokeza wanawake wengi kugombea uongozi kuanzia ngazi ya vijiji, vitongoji na mitaa.

"Naomba wanawake wenzangu tujenge imani ya kuaminiana na tuungane mkono, tuache tabia ya kutoaminiana," alisema Ndege.

Mmoja wa wajumbe wa kikao hicho, Ngaisi Mollel, alisema ujumbe huo ni mzuri kwa wanawake, hivyo wajitokeze kuchukua fomu za kugombea uongozi.

Mollel, aliahidi kufikisha ujumbe huo hadi kwenye ngazi ya vitongoji kwa wanawake ili wengi zaidi wahamasike kugombea nafasi hizo.

"Tunatarajia wanawake wengi zaidi kujitokeza kugombea nafasi za kugombea uongozi wa serikali za mitaa pindi muda wa uchaguzi utakapofika," alisema.





# DC aamuru mkandarasi anyang'anywe zabuni

Na Marco Maduhu, SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Julius Mtatiro, ameagiza mkandarasi wa Kampuni ya Fomast anayetekeleza ujenzi wa daraja anyang'anywe kazi hiyo kutokana na utendaji kazi wake kutoridhisha.

Alitoa agizo hilo juzi akiwa ameambatana na wajumbe wa Kamati ya Ulinzi ya Wilaya ya Shinyanga pamoja na wataalamu kutoka Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA).

Mtatiro alisema serikali wilayani Shinyanga haitokuwa tayari kuwapa kazi makandarasi wasiotekeleza miradi yao kwa mujibu wa mikataba na kwamba mkandarasi huyo anyang'anywe kazi hiyo.

"Mkandarasi huyu ambaye anatekeleza ujenzi wa barabara na daraja kuunganisha Kata ya Mwawaza, Chibe na OldShinyanga, naagiza kazi ya daraja anyang'anywe apewe mtu mwingine, yeye abaki na barabara tu, Jumamosi nipewe mpango kazi wake wa ukamilishaji wa barabara hii," alisema Mtatiro.

Katika hatua nyingine, Mtatiro aliagiza ufanyike utaratibu mzuri wa namna ya kuwaelemisha na kuwaondoa wananchi wanaofanya shughuli za kilimo pembezoni mwa Mto Ning'wa eneo ambalo litajengwa daraja hivi karibuni.

Kaimu Meneja wa TARURA Wilaya ya Shinyanga, Yohana Williamu, alisema mkandarasi huyo kazi zake zimekuwa za kusuasua na kwamba wamekuwa wakizungunza naye kumhimiza kuongeza kasi lakini bado hali iko vilevile.

Hivyo, aliahidi kutekeleza maagizo ya Mkuu wa Wilaya ya kumnyang'anya kazi ya daraja hilo.

Awali akizungumza wakati wa ziara hiyo, mkandarasi kutoka Kampuni ya Fomast, Exavel Mapunda, alisema ameshindwa kuendana na kasi ya ujenzi kutokana na awali kukabiliwa na changamoto ya mvua.

Aidha, Mtatiro alikagua barabara na daraja zinazounganisha Kata ya Mwasele, Ndala, Mwawaza na Chibe hadi kwenda OldShinyanga, Butengwa.

Pia alikagua ujenzi wa barabara za majengo mapya pamoja na katikati ya mji ambazo zinajengwa kwa kiwango cha lami.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (wa pili kushoto), akisikiliza maelezo kutoka kwa Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya Muhimbili (MUHAS), Dk. Nathanael Sirili (kulia), kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Kampasi ya chuo hicho Kanda ya Magharibi, alipotembelea kukagua eneo la ujenzi wa mradi huo, mkoani Kigoma juzi. **PICHA: OMR**

# Wachimbaji madini hatarini kupata magonjwa mlipuko

Na Shaban Njia, KAHAMA

WACHIMBAJI wadogo wa mgodi wa Nyikoboko Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga wako hatarini kupata magojwa ya mlipuko kutokana na kujisaidia vichakani.

Hali hiyo imebainika mgodini hapo wakati wa ziara ya Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa kimadini Kahama, Joseph Kumburu, wakati akikagua hali ya usalama wa migodi pamoja na kusikiliza kero mgodini hapo.

Mmoja wa wachimbaji hao, Maganga Emmanuel alisema hali ya mgodi huo ni mbaya kwani hakuna vyoo na wanajisaidia vichakani, hali inayohatarisha afya zao na kuiomba serikali iingilie kati na kutatua shida hiyo.

"Tunajisaidia vichakani kwasababu hakuna vyoo mgodini kwetu, leo hakuna mvua ila zitakapoanza kunyesha hali itakuwa mbaya na tutapata magonjwa ya kuhara na kipindupindu, tunalazimika kujisaidia kwenye vyoo vya nyumba jirani vinayozunguka mgodi huu," alisema Emmanuel.

Mfanyabiashara wa chakula katika mgodi huo, Rehema Hasan alisema biashara ya chakula imekuwa ikiendelea katika maeneo hayo licha ya hali hiyo, hivyo kuomba yajengwe hata matundu mawili kwa ajili ya kumudu jinsia zote.

Meneja wa mgodi huo, Charles Izengo alikiri kutokuwapo kwa huduma ya vyoo mgodini lakini wameshaanza kuchukua hatua za haraka kwa kuanza kuchimba shimo na kujenga vyoo vya kisasa.

Hivyo, aliwataka wachimbaji kutumia vyoo vya nyumba za wageni huku wakiendelea na ujenzi na kuacha kujisaidia vichakani.

Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Kimadini Kahama, Joseph Kumburu, aliutaka uongozi wa mgodi kuhakikisha wanajenga vyoo vya kisasa ili kuondoa kero hiyo.

## Mganga Mkuu atoa maagizo matatu watumishi afya

Na Vitus Audax, MWANZA

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Jesca Lebba, amewataka watumishi wa sekta ya afya mkoani hapa kuhakikisha wanafuata sheria, kanuni na taratibu za kazi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Amesema lengo ni kutoa huduma stahiki na kufikia malengo yaliyowekwa.

Dk. Lebba alitoa kauli hiyo juzi wakati akikabidhiwa ofisi na aliyekuwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza ambaye kwa sasa amehamishiwa Mkoa wa Dodoma, Dk. Thomas Rutachunzibwa.

Dk. Lebba ambaye amehamishiwa mkoani hapa akitokea Mkoa wa Kigoma aliwataka watumishi hao kutoa ushirikiano na kufanya kazi kwa weledi ili kuzidi kutoa huduma bora katika sekta ya afya.

"Ninajua mna ushirikiano tangu hapo awali lakini tushirikiane zaidi na zaidi kwani tuongeze kasi ya mafanikio na pia tufanye kazi zenye matokeo halisi," alisema.

Aidha, aliwataka viongozi na wasimamizi mbalimbali wa idara ya afya walioshiriki katika makabidhiano ya ofisi kuendelea kufanya kazi kama timu, akisema kwa kufanya hivyo kutarahisisha kazi.

Aliyekuwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Thomas Rutachunzibwa, alisema ameiacha ofisi katika mikono salama kwani anamfahamu vizuri Dk. Lebba na anaamini katika ufanisi wa utendaji kazi wake, hivyo kutaka apatiwe ushirikiano wa kutosha.

Alisema: "Ninaamini tulishirikiana vizuri sana na ninawaombeni mumpatie ushirikiano wa kutosha Dk. Lebba kama mliokuwa mkinipatia mimi".

## DC aagiza wanaokwepa chanjo wafichuliwe

Na Halima Ikunji, TABORA

MKUU wa Wilaya ya Sikonge, Cornel Magembe, amewaagiza viongozi wa serikali za vijiji na watendaji wa kata kuhakikisha wanawafichua wafugaji wanaoficha ng'ombe wasipewe chanjo.

Alitoa agizo hilo juzi wilayani hapa wakati wa utoaji chanjo ya kudhibiti ugonjwa wa mapele kwa ng'ombe 14,000 katika kata nne.

Alisema kwa kipindi cha miaka miwili zoezi hilo limekuwa likifanyika katika wilaya nzima na likiwa na matokeo chanya yaliyosababisha kuongezeka kwa mifugo ikiwamo kudhibitiwa ugonjwa huo uliokuwa ukisababisha ng'ombe kufariki.

"Yeyote atakayebainika kuficha mifugo au kukwamisha zoezi hili kwa namna yoyote ile atachukuliwa hatua kali za kisheria, tunataka mifugo yote ipate chanjo hii na magonjwa mengine yadhibitiwe pia," alisema.

Ofisa Mifugo wa Wilaya hiyo, Maulid Rajabu alisema kwa mwaka 2021/22 walichanja ng'ombe 99,303 na 2022/23 walichanja ng'ombe 112,116.

Mfugaji kutoka Kata ya Ngoywa, Mao Maganga, alisema chanjo hiyo imekuwa msaada katika kudhibiti vifo vya mara kwa mara kwa mifugo yao na kuahidi kuwaelimisha wanaoficha mifugo ili ipewe chanjo.

ama
ALHAMISI JULAI 11, 2024
AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 12

**Ubunifu wa wanachuo – DIT kidhibiti mbu kinachoendana na maisha nchini**



**Siku ilipokuwa tabasamu la wanaolelewa vituoni, kutokana na magumu makwao**

Ukurasa 13

## SHIDA KIWANDA CHA KUPATA MTOTO...

# Bingwa tiba JWTZ, afunguka yanayofuata mtoto akizaliwa korodani zake hazishuki

## •Atoa kanuni za ukaguzi kwa 'Mzaa Chema'

**Na Beatrice Shayo, ARUSHA**

DAKTARI Bingwa wa Magojwa ya Watoto, kutoka Hospitali ya Jeshi Monduli, mkoani Arusha, Emmanuel Luchagula, amezitaja sababu za korodani kushindwa kushuka chini kwenye vifuko vyake mtoto akiwa tumboni, hata baada ya kuzaliwa.

Anataja huku akisisitiza kwamba, endapo zikiachwa kuendelea kubaki, kuna uwezekano wa kusababisha uvimbe ikiwamo maradhi ya Saratani.

Dk. Luchagula, ni miongoni mwa madaktari bingwa waliokuwa wanatoa huduma bure kwa wananchi katika kambi maalum iliyofanyika kuanzia Juni 24 hadi Julai Mosi mwaka huu, iliyoandaliwa na Mkuu wa Mkoa Arusha, Paul Makonda maarufu 'Kambi ya Makonda' .

Wakiwa wanatoa huduma, walibaini watoto 10 ambao korodani zao bado zipo tumboni hazijashuka chini, wamepatiwa rufani ya kwenda Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), kufanyiwa upasuaji wa kuzishusha.

Akizungumza na Nipashe, Dk. Luchagula, anaeleza kuwa korodani hizo zikiendelea kubaki tumboni, huzalisha uvimbe baada ya muda na kuna uwezekano wa kusababisha Saratani.

Anasema, pia kuna uwezekano wa mhusika kushindwa kupata mtoto wanapokuwa watu wazima ni mkubwa, kutokana na korodani hizo kubaki tumboni.

Mtaalamu huyo anaeleza kiundani kuwa mtoto anapoumbika tumboni, kuna seli zinazogawanyika katika makundi matatu.

"Kundi la kwanza ni Seli aina ya 'Endoderm' yenyewe inashughulika na uumbaji wa viungo vya ndani, baadhi sio vyote. Lakini, kuna seli nyingine inaitwa 'Ectodem', inahusika kuumbika kwa ngozi na viungo vyake ikiwamo vinyweleo," anasema

Anataja seli ya kundi la tatu ni 'Mesoderm' inayohusika kutengeneza mfumo wa moyo, mishipa ya damu na viungo vingine vya ndani.




DAKTARI Bingwa wa Magojwa ya Watoto, kutoka Hospitali ya Jeshi Monduli, mkoani Arusha, Dk. Emmanuel Luchagula. **PICHA: BEATRICE SHAYO.**

### KORODANI ZINAVYOOUMBIKA

Dk. Luchagula anasema, korodani hizi zinaumbika 'nusu ya Ectoderm' na 'nusu ya Mesoderm' na zikiungana kwa pamoja zinatengeneza kinachoitwa 'Intermediate Genital Ridge', inayotengeneza korodani.

Anasema, korodani katika hatua za awali za kuumbika kwake, kimsingi huwezi kujua kama mtoto ni wa kike au wa kiume, kwa sababu na zenyewe zinakuwa tumboni kama inavyokuwa kiwanda cha kutengeneza mayai yaani (ovary) kwa mtoto wa kike, kipo tumboni.

"Hizi zinakuwa kama mfumo wa 'ovari' lakini tunasema mtoto anavyoendelea kukua ama kuumbika kwa viungo vya ndani kunaanza kutengenezwa kwa mifumo tofauti tofauti na mifumo hiyo inategemea udhibiti wa (homoni) ama vichocheo," anasema.

Dk. Luchagula anaeleza kuwa, homoni zinazohusika na jinsia ya kike au kiume anaziita kitaalamu 'Anti mullerian' homoni (AMH) na 'Testosterone.'

Anasema ni homoni zinazochochea au kuzuia maumbile mengine yasiendelee, maana yake vichocheo hivyo vina sehemu kubwa kumfanya mtoto wa kiume kuonekana maumbile yake ya ndani au nje kama vile yalivyo.

### JINSI ZINAVYOSHUKA

Dk. Luchagula anasema, kwa kawaida korodani zinatakiwa kushuka kutoka tumboni kuanzia wiki ya nane mpaka 15 tangu mimba ilivyotungwa.

"Kutengenezwa kwake zinaanza wiki ya nne hadi ya saba na huwa zinategemea homoni nilizozieleza, ambazo zinachochea kuharakisha mchakato na process ya kwanza ya kutengenezwa ni kukomaa na kuanza kushuka kutoka tumboni," anasimulia.

Anasema, isipokuwapo homoni ya Antimuleriani korodani zinapevuka kuwa ovari na kubaki huko tumboni.

Dk. Luchagula anasema mpaka mtoto anapokuja kuzaliwa inatakiwa korodani ziwe zimeshuka, kuna asilimia ndogo ya watoto jambo hilo huwa linachelewa na kukwama njiani.

Anafafanua, katika idadi ya watoto wa kiume wanaozaliwa, changamoto hiyo ya kiafya kuchelewa kushuka korodani, ni ndogo wastani asilimia saba.

Dk. Luchagula anataja sababu ya korodani kubaki tumboni, inasababishwa na mambo mbalimbali ikiwamo vichocheo (hormones) au vinasaba (genetics).

"Hitilafu wakati wa kuumbika kwa viungo (Organogenesis defect), upo uwezekano wa korodani kutoendelea kukomaa, ikaishia njiani na kubaki tumboni.

"Maana yake ni kwamba inapoteza sifa, inakuwa kitu kingine. Kuna hatua mbili, yaani tumboni na kwenye uvungu wa nyonga (Inguinal/groin)," anaeleza.

Anasema kuna baadhi ya watoto korodani hushuka toka tumboni, ikishafika eneo la chini karibu na nyonga (Inguinalscrotal) hukwama hapo, akilitolea ufafanuzi: "Kwa huyu kuishusha ni rahisi kuliko yule ambaye bado ipo tumboni,".

### WAZAZI KUFAHAMU

Mtaalamu huyo anasema, mzazi anatakiwa kushirikiana na wataalamu watoa hudumu za afya, pale mtoto anapozaliwa. ili kumkagua kwa kuzishika korodani.

"Unaweza kuona mbona korodani moja haipo, unatakiwa kujua vigololi vyote viwili vipo au

Inaendelea Uk. 13

AFYA

# Ubunifu wa wanachuo – DIT kidhibiti mbu kinachoendana na maisha nchini

**Na Beatrice Philemon**




Joel Ngushwai, Mratibu kutoka studio ya Taasisi DIT akionyesha jinsi kifaa hicho kinavyofanya kazi, katika Maonyesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba), Dar es Salaam wiki hii. **PICHA: BEATRICE PHILEMON.**

BAADA ya kuona mbu ni zaidi ya kero nchini kama vile kwenye Malaria, Homa ya Dengue na Virusi vya Zika, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) imetengeneza kifaa cha kuwaua kutumia mwanga uitwao Ultraviolet (UV).

Ni kifaa kimepewa jina la 'Mosquito Killer for Killing Harmful Insects' kuua mbu na kupunguza mzigo wa magonjwa nchini.

Kilivyoundwa kinawavutia mbu kwa kutumia njia mbalimbali; mwanga na joto. Kina uwezo kuwavutia mbu umbali wa mita 90 iliko mwanga na huwekwa ndani ya nyumba, kwenye uwazi kama vile hospitali, maeneo ya mapumziko kwenye mabweni, shule na vyuoni kutumika kuua mbu.

Akizungumza na Nipashe kwenye Maonyesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba), Joel Ngushwai, Mratibu kutoka Studio DIT, anasema ni kifaa kinachotumia teknolojia maarufu sana kwa kudhibiti mbu.

Ni kifaa cha kwanza kutengenezwa na baada ya kuona kinafanya kazi, kumeshafanyika majaribio ndani ya maeneo ya DIT, Dar es Salaam, kwa muda wa mwezi mmoja na wamegundua ina uwezo wa kuua wadudu wengi warukao kwa asilimia 95.

"Kwa mtu, chuo au hospitali anayetaka kutumia kifaa hiki kupambana na mbu, kuna njia mbili. Ya kwanza, anaweza kutumia 'solar' (nguvu ya jua) na njia ya pili anaweza kutumia umeme." anasema.

Wameamua kutengeneza kifaa hicho, baada ya kuona uwapo wa mbu wengi katika baadhi ya hospitali na vyuo, wakazi wakihangaika kupambana na mbu.

Anasema, kifaa hicho kimekuwa maarufu na suluhisho la kupambana na wadudu warukao, kwani ina njia rahisi na rafiki kwa mazingira kupunguza mbu, mijini na vijijini.

### FAIDA KWA JAMII

Kupunguza mbu katika jamii, inatajwa kusaidia kuondoa mzigo wa magonjwa yanayosababishwa na mbu katika jamii, hali inayowezesha kupunguza waendao hospitalini na kliniki kwa matibabu kama malaria.

Watengenezaji DIT, wanajivuna kifaa kitawasaidia watumiaji kupunguza kelele, pia kuumwa na mbu, hata usalama wa watoto na watu wazima dhidi ya magonjwa tajwa.

Pia, wanataja ni suala linalotoa amani ya akili, kujua kinga dhidi ya mbu na magonjwa wanayosababisha, katika tafsiri kutoa amani ya akili, hasa msimu wa mvua wenye mbu wengi zaidi.

Kibiashara, kunatajwa ushindi wa vita dhidi ya mbu kunavutia wageni kibiashara kama vile watalii zaidi.

"Mtu ambaye atapenda kutumia kifaa hiki kwa ajili ya kuua mbu lazima hahakikshe kifaa hiki kinawekwa kwenye maeneo yasiyoweza kufikiwa kwa urahisi na watoto wadogo na wanyama vipenzi wa binadamu, ili kuepuka ajali zinazoweza kutokea kama vile kugusana na gridi ya umeme au kuangusha kifaa," anasema Ngushwai.

### TEKNOLIJIA YAKE

Inatajwa kuwa kifaa kinachotumia mwanga wa ultraviolet (UV) kuvutia mbu, wakati mbu wanaporuka kuelekea kwenye mwanga, wanagusana gridi iliyo ya umeme na inawaua papo hapo.

Teknolojia hiyo ya kuua mbu, inatajwa kuwa maarufu kutokana na ufanisi wake, katika namna kadhaa:

Mosi, inavutia na kuua mbu ufanisi mkubwa na wanapokaribia chanzo cha mwanga, wanagusana na gridi ya umeme inayowaua papo hapo.

Pia, matumizi ya kifaa hicho, kina nafasi ya kupunguza magonjwa yanayosababishwa na mbu nchini, Tanzania ikiwa katika orodha ya waathirika na malaria, pia kuwapo magonjwa mengine kama Homa ya Dengue na virusi vya Zika.

Kuna suala la kupunguza mbu kwa kutumia kifaa hicho, kinawanusuru watoto walio hatarini kuathirika ama na malaria au magonjwa mengine yanayosababishwa na mbu; kifaa hicho kinapoua mbu nyumbani na kulinda afya ya watoto.

Watalamu DIT, pia wanataja kupunguza matumizi ya kemikali: Badala ya kutumia vizuia wadudu vya kemikali vinavyoweza kuwa na madhara kiafya, ni kifaa kinachotoa njia salama na bora kudhibiti mbu.

### FAIDA YA MAZINGIRA

Vifaa vingi vya kuua mbu sasa kimuundo, vinakuwa rafiki wa mazingira. Mitego ya asili na isiyo na sumu inaepuka kemikali hatari, hata kuifanya salama kwa mazingira.

Pia, vifaa vinavyotumia nishati ya jua (solar) vinapunguza matumizi ya umeme na kusaidia kuokoa nishati.

Hiyo inafanyika kwa staili ya kupunguza matumizi ya dawa za kuua wadudu: kifaa cha kuua mbu kinaweza kusaidia kupunguza utegemezi wa dawa zinazoweza kuwa na athari mbaya kwa mazingira na viumbe vingine.

Kulinda viumbe wengine: Inachagia kuepuka matumizi ya kemikali kali, kifaa kinachosaidia kuhifadhi viumbe hai vingine, kama wadudu muhimu bustanini, ndege, na wanyama porini.

### GHARAMA NAFUU

Gharama za Muda Mrefu: Katika uwekezaji wa awali kwenye kifaa cha kuua mbu, mtu anaweza juu kuliko vinavyozuia wadudu vya kawaida, akiba ya muda mrefu ni kubwa.

Hiyo inaendana na kupungua gharama za matibabu ya magonjwa yanayosababishwa na mbu muda wa Maisha, vifaa vinavyochangia kuwapo akiba ya jumla.

Kwenye umeme, mashine nyingi hivi karibuni hutumia nishati ya jua (solar), hivyo kupunguza gharama za umeme na ziko rafiki wa mazingira.

Kuna eneo la kupunguza matumizi ya vizuia wadudu: Ni kifaa kinachopunguza hitaji la kununua na kutumia vizuia wadudu kila mara, hivyo kuokoa gharama kwa muda.

### URAHISI WA MATUMIZI

Ni kifaa ambacho kwa ujumla, kiko rahisi katika matengenezo yakihitajika kidogo na kinatoa suluhisho lisilo na matatizo kwa udhibiti wa mbu unaoendelea, kuruhusu ufurahiaji maeneo ya ndani na nje bila kero ya mbu.

Kinatajwa kuwa kifaa kinachohitaji matengenezo mengi. Kwa mfano, vianzishi umeme husafishwa kila mara kuondoa mabaki ya mbu waliouawa, wakati mitego yake inahitaji kujazwa mitungi yenu hewa ya ukaa.

Pia, ni kifaa kisicho na harufu, hivyo kuifanya iwe rahisi kutumia ndani ya nyumba na maeneo ya nje.

Kisaikolojia, ni jambo linalotoa kinga kwa magonjwa hasa msimu wa mvua mbu wakiwa wengi zaidi.

### UDHIBITI KASORO

Watalamu hao wanaeleza, ikiwa kifaa chako hakifanyi kazi, angalia kama kimeunganishwa vizuri kwenye chanzo cha umeme.

Pia, hakikisha nyaya zote ziko salama na kuna umeme wa kutosha na ikiwa kifaa kinatumia betri, angalia kama zina nguvu ya kutosha na kufanyiwa utatuzi.

Inaelezwa, ni kifaa hakitoi mwanga wa UV, balbu inaweza kuwa imeharibika au kuna tatizo na mfumo wa umeme. Mhusika anatakiwa abadilishe balbu na kuona kama tatizo linaendelea.

Ikiwa bado haitoi mwanga huo, inadhauriwa inangaliwe nyaya na vyanzo vya umeme kwa matatizo yoyote na ikiwa kifaa hicho kinatoa harufu mbaya, mhusika anaweza kuwa na mabaki ya mbu waliokufa ambao hawajaondolewa kwa muda mrefu.

Suluhisho linatajwa ni kusafisha na kupata kifaaa vizuri, kuhakikisha hakuna mabaki yonayobaki kwenye gridi ya umeme.

Hiyo inatokana na kufuata vidokezo vya uwekaji na matengenezo, kuhakikisha kifaa kinaua mbu na kinafanya kazi kwa ufanisi wa muda mrefu.

Kifaa hicho kinawekewa muhimu wa afya na faraja, huku katika suala la matengenezo sahihi, inaaweza kusaidia kupata matokeo bora zaidi.

AFYA

# Siku ilipokuwa tabasamu la wanaolelewa vituoni, kutokana na magumu makwao

**Na Yasmine Protace, KIBAHA**



Halfa mojawapo ya kutoa msaada katika kituo cha yatima wilayani Kibaha. **PICHA: MTANDAO.**

VITENDO vya ukatili wa kijinsia unaofanywa na jamii dhidi ya watoto, unajulikana watoto kuishi katika makao ya kulea watoto yatima.

Hivi karibuni katika sherehe mojawapo kutoa sadaka kwa makao tisa ya watoto yatima mjini Kibaha mkoani Pwani, Ofisa Ustawi wa Jamii, Faustina Kayombo, anasema changamoto za kifamilia ambazo ndizo chanzo cha watoto kuishi katika vituo vya kulea watoto yatima.

Anasema, katika Halmashauri ya Mji Kibaha, kuna makao tisa ya kulea watoto yatima ikiwa na idadi ya watoto zaidi ya 600.

watoto kukaa katika makao hayo, ni pamoja na kubakwa, kulawitiwa, kukimbiwa na wazazi na ugumu wa maisha.

Anasema katika makao hayo tisa yote yaliyosajiliwa, anapasifu ambako hayo yamekuwa mkombozi kwa watoto hayo kutokana na kulelewa huku wakipatiwa fursa za masomo.

Kayombo anasema, kuwalea watoto na kuwapatia mahitaji, inatakiwa jamii ijitokeze kuwasaidia watoto hao na sio kuiachia serikali pekee.

" Watoto wanahitaji faraja, hivyo wanapokumbukwa kwa zawadi yoyote wanafarijika," anasema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halamshauri ya Mji wa Kibaha, Dk Rogers Shemelekwa, anasema kuwa watoto wako kama wengineo, hivyo kuwapa sadaka ni jambo jema.

Anasema, katika kipindi cha mwaka wa fedha mwaka huu, walitafakari na kuona kuna haja ya kuwasaidia yatima, akinena kisaikolijia, watoto hao nao wangependa kuwa na familia zao, lakini kutokana na mambo mbalimbali yanayojitokeze wanabaki katika maisha ya yatima.

"Makao haya wanafanya kazi kubwa kuwalea watoto, hivyo jamii nayo inatakiwa kujitoa sadaka kwa yatima ili nao wafurahi," anasema.

Anaongeza kuwa, hata Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amekuwa mstari wa mbele kutoa sadaka katika makao ya Watoto aina hiyo.

Anasema, halmashauri yao kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, wametoa sadaka kwa watoto wa vituo hivyo yenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni nne.

"Tumeguswa na watoto, hivyo tumetoa sadaka yetu kwa watoto wa vituo tisa ili waweze kufurahi kama wenzao," anasema.

Anaongeza kwamba katika kutoa sadaka hiyo, wameambatana na kamati ya ulinzi na usalama wazee wa dini, madiwani na viongozi wa watu wenye makundi maalumu, pia wasanii.

Anasema kutokana na Rais Dk. Samia kufanya makubwa katika Mji Kibaha ndani ya miaka mitatu ya uongozi wake, wamefanyia maombi makubwa afanikiwe zaidi.

"Viongozi wa dini na watoto wa makao wamemfanyia maombi Dk. Samia," anasema na kufafanua kwamba, watoto hao ni familia moja, hivyo, kuna wajibu wa kuwasaidia na sio kuiachia serikali pekee katika utoaji misaada kwao.

Mwakilishi wa Mbunge wa Mji Kibaha, Joseph Jackson, anasema Mkurugenzi wa Halmashauri alichokifanya ni cha kilele na kiafa mkoani Pwani.

"Nina miaka zaidi ya 20... sijawahi kukiona hiki kitu kufanywa na wakurugenzi (DED), hivyo naona wakurugenzi wengine wanatakiwa kuyaiga haya," anasema

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Kibaha, Mussa Ndomba, anawapongeza wadau waliofanikisha kupatikana misaada hiyo.

Mussa anasema kuwa, wamejikita katika kuhakikisha watoto hao wanapata elimu kama ilivyo kwa watoto wanaoishi na familia zao kwani hiyo ni haki yao.

**KUTOKA VITUONI**

Jamila Juma, kutoka Kituo cha Shallom, anaelekeza shukurani kwa waliojitoa na kuwasaidia mahitaji ya shule, ikiwamo kuwakutanisha na watu mbalimbali kwao ni faraja tosha.

" Watoto yatima tunapitia changamoto nyingi,majumbani na ndio maana tunalelewa vituoni, lakini tunawashukuru wote kwa kutujali kwa misaada yao," anasema.

Hamis Jabiri, mtoto kutoka kituoni hapo, anaelekeza shukurani kwa serikali kuwajali na kuwatambua, pia kwa sadaka zilizotolewa.

"Tunakaa katika vituo kutokana na changamoto tunazozipitia kwetu," anasema, akiendelea kuwa, kila mtoto aliyepo kituoni anaposimulia kilichomleta hapo, mtu anajisikia vibaya, hivyo wanawashukuru wanaowasaidia mahitaji ya shule na vyakula.

"Hapa kila mmoja ana changamoto yake. tukianza kusimulia, tunajisikia vibaya kwa mambo ya ukatili ambayo yanafanyika majumbani," anasema.

Mmoja kutoka kituo hicho cha Shallom kilichopo Mkuza, Kibaha, anasema kituo chao kina watoto waliowapokea wakiwa na miaka miwili na sasa wamekuwa na wanaendelea vizuri.

Anasema baadhi yao waliowapokea, wakiwa wamebakwa na wazazi, walezi, wapo waliolawitiwa majumbani na wengine wazazi wametengana na kukosa mtu wa kumlea.

## Bingwa tiba JWTZ, afunguka yanayofuata mtoto akizaliwa korodani zake hazishuki

**Inatoka Uk. 11**

kuna kigololi kimoja," anasema.

Anasema, kuwapo gololi moja, huenda ilitengenezwa yenyewe moja kitaalamu, wanashauri kumfanyia mtoto uchunguzi kukagua, kama itakuwa tumboni au imekwamia njiani.

Mtaalamu huyu anasema, kitaalamu mtoto akizaliwa bila ya korodani moja, inashauriwa ndani ya miezi sita korodoni ziwe zimeshaondolewa ndani ya tumbo na sababu ya kuishusha mapema kile, ni kiwanda cha kutengeneza mbegu, kinaathiriwa na joto la tumboni.

"Kile kiwanda hakihitaji joto. Mungu alivyoziweka chini hakuwa anataka zisipate joto kali kama la mwili. zinatakiwa kupata joto pungufu la mwili kwa nyuzijoto mbili hadi saba, ndio maana wakati wa baridi kali zinarudi ndani hazitaki ubaridi sana wala joto kali," anasema

**WAGONJWA WAKE**

Dk. Luchagula anasema kati ya watoto 10 waliobainika kuwa korodani zipo tumboni, wana zaidi ya umri wa miaka mitano, wengine mitatu na miwili.

Anafafanua kwamba, zikichanwa korodani hizo ndani ya tumbo zina tabia ya kubadilika na kuwa uvimbe badala ya korodani na kusababisha uwezekano wa kupata ugonjwa wa saratani.

"Wasi wasi mkubwa uvimbe unabadilika kuwa saratani utakuja kusikia wakisema ana uvimbe tumboni bila kuja ni ile korodani ambayo haikuonekana sasa kwa hawa Watoto, ni lazima zishuke korodani zilizopo tumboni," anasema

Anarejea tafiti mbalimbali, kwamba kama mtoto anachelewa kufanyiwa upasuaji, haitakiwi kuzidi miezi 18 wanachokifanya ni upasuaji.

Bingwa huyo anasema, anaweza kufanyiwa upasuaji kwa mara mbili, awamu ya kwanza ni kuishusha na baada ya muda wa miezi sita au mwaka, inategemea na kile kitaonekana na kwenda katika awamu nyingine ya kushusha korodani.

**USHAURI WAKE**

Dk. Luchagula anawashauri kinamama wanapojifungua watoto wa kiume. kuhakikisha wanawakagua akinena: "Sasa wazazi wengine hata akishika hajui kama hizo gololi zipo mbili ama ni moja wengine ni mambo ya mila na desturi hawaruhusiwi kuchungulia,".

Anasema, kama kuna gololi moja iliyoshuka kuna uwezekano wa kufanya kazi na kuwa na uwezo wa kuzalisha akifafanua:

"Maana yake, atakuwa na kiwanda kimoja ambacho kinafanya kazi ikitokea, ina uwezo mdogo. Uwezekano wa kukosa mtoto ni mkubwa kwenye uzazi kinachozingatiwa ni ubora wa mbegu."

Anasema wapo wanaume ukiwatizama maumbile wapo sawa, lakini hawana uwezo wa kuzalisha au kusababisha mimba "Mwanaume kusimamisha na kuzalisha ni vitu viwili tofauti.".

MAZINGIRA

# Mfumo wa 'Taka Sifuri' unavyohamisha uchafu, kuwa neema mazingira, kipato

**Na Halfani Chusi**

INAWEZEKANA kumaliza tatizo la taka kwa kutumia mfumo wa taka sifuri, iwapo utaenezwa nchi nzimaa.

Mfumo huo umeshaleta mafanikio kadhaa nchini, kwa baadhi ya maeneo unakotumika sasa wanafurahia matunda yake.

Hata hivyo, bado kuna maeneo hautumiki ni ama kwa kutokujua au kukosekana nyenzo muhimu za kufanikisha urejelezaji wa taka na mfumo wake kwa ujumlakwa namna ya kubadili taka kuwa mali.

Katika kufanikisha hilo, Taasisi ya Nipe Fagio nchini inayojihusisha na udhibiti wa taka kwa kueneza mfumo wa taka sifuri imewakutanisha wadau mbalimbali duniani katika Mkutano wa Kimataifa wa Miji ya Taka Sifuri walioundaa kwa kushirikiana na Mtandao wa Vikundi vya Wananchi (GAIA).

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi hiyo, Anna Rocha katika mkutano huo, anaanza kwa kutaja dawa ya kufanikiwa katika hilo kuwa ni pamoja na ushirikiano baina ya jamii, taasisi zisizo na kiserikali na serikali yenyewe.

Mkurugenzi huyo anaeleza kuwa baadhi ya maeneo nchini kama Dar es Salaam, Tanga, Arusha, Zanzibar wamefanikiwa kudhibiti taka kwa kutumia mfumo huo.

Mkurugenzi huyo anasema, wakati wanaanza kuutumia mfumo huo nchini walitathmini uhalisia wa mazingira na maisha ya Watanzania na kubaini ni rafiki na hauna gharama.

Pia, tathmini hiyo, ilitoa jawabu la mifumo gani ibuniwe kulingana na uhalisia wa maisha ya Tanzania na hali yake kiuchumi, ili kudhibiti taka.

"Kupitia hiyo tumeweza na hivi sasa Tanzania ni moja ya nchi zinazofanya vizuri Afrika kudhibiti taka," anasema Anna.

Anasema msingi wa juhudi zote hizo ni kuhakikisha Tanzania na dunia kwa ujumla inakuwa mahali pazuri kuishi palipo tawaliwa na hewa safi.

Anna anasema pia walijadiliana kuhusu mabadiliko ya tabianchi kwa kuwa ni jambo linalo shabihiana na taka.

"Hakuna mtu anayeweza kuboresha maisha peke yake, ni lazima tuboreshe kwa pamoja, hiyo ndiyo sababu tupo na watu wengi hapa," anasema.

Mkurugenzi huyo anaendelea na ufafanuzi wake kwamba: "Watu wanapopewa uchaguzi mzuri, wanauchukua. Taka Sifuri sio suluhisho tu; ni dhamira ya mustakabali shirikishi kwa Tanzania, Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwingineko.

"Mfumo wa Taka Sifuri unapendekeza mifumo itakayotatua matatizo ya kimazingira kama uchafuzi wa hali ya hewa, kuruhusu jamii kuelewa mienendo yake na kuchukua hatua stahiki katika kushughulikia matatizo yao" anasema



Uchafu ukiwa mtaani na kuwa kero kwa afya. **PICHA: MTANDAO.**

Anafafanua kwamba, mfumo huu unaotekelezwa nchini ni jitihada za wazi unaoshirikisha jamii wenye mafanikio unavyoweza kuigwa na kuingizwa katika mazungumzo ya kitaifa, kukuza haki ya kijamii, na kuleta mabadiliko katika utekelezaji wa usimamizi wa taka katika miji na nchi nyingi za Afrika.

Anaongeza Kupitia mfumo huo wamefikia kiwango cha asilimia 95 cha utenganishaji wa taka katika maeneo ya Dar es Salaam na Arusha anasisitiza inamaana kwamba asilimia 95 ya watu wanaoioshi katika jamii ya kipato cha chini wamekubali kutenganisha taka zao katika makundi yaliyoamuliwa awali kuwezesha viwango vya juu kurejeleza taka.

Anapochangia mada katika mkutano huo, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Serikali za Mitaa Zanzibar, Mahmoud Mussa anasema utekelezaji wa mpango wa taka sifuri visiwani humo unalenga kuviweka safi visiwa hivyo.

Hapo anakumbushia kwamba mzizi wa uamuzi huo ni kile alichoeleza, tangu Rais Hussein Mwinyi aningia madarakani aliweka wazi kutoridhishwa na hali ya uchafu ndani ya mji.

"Ile ilikuwa ni kauli mbiu kuhakikisha tunakwenda tunafika hatua tunaondoa tatizo la uchaguzi Zanzibar," anasema.

Ili kufanikisha hayo, anasema alikutana na wadau mbalimbali wenye uelewa na uzoefu wa mpango huo na kwamba hatimaye alieleweka.

Katika ufafanuzi wake, anasema alilazimika kuchukua vijana kutokea visiwani Zanzibar kuwaelimisha juu ya usafi na hatimaye alifanikiwa.

Haikuishia hapo, anasema walijenga maeneo ya kukusanyia taka Mjini Magharibi na kwa sasa mpango uliopo ni kujenga vituo vingine sita.

Anasema kwa sasa anatarajia kuzitumia taka hizo kuwa rasilimali na hatimaye ziwe fursa badala ya uchafu.

Anatamba mpango huo haulengi eneo lake pekee, bali maeneo yote ya visiwa vya Zanzibar.

Mratibu wa Miradi ya Ufadhiri Kutoka Benki ya Dunia kwa kushirikiana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini nchini (TARURA), Humphrey Kanyenye katika mkutano huo anaisihi jamii kushirikiana kufikia malengo ya taka sifuri.

"Tunauwezo wa kupunguza taka kwa kutumia vikundi mbalimbali vilivyopo kwenye jamii zetu kwa kukusanya, kuchakata na kupata mbolea inayoweza kutumika katika kilimo, viwavi kwa ajili ya chakula cha kuku.

Hivyo, sisi kama TAMISEMI na TARURA wenye Miradi inayoendelea hasa katika Mkoa wa Dar es salaam ujuzi huu umetuongezea faida nyingine," anasema Kanyenye.

Anasema kupitia Mradi wa uendelezaji wa Mkoa wa Dar es Salaam (DMDP) wameanza na taasisi ya Nipe Fagio na kwamba mpango uliopo ni kuanzisha mfumo wa usimamizi wa taka ngumu.

"Hii njia wanayoitumia wenzetu wa mataifa mengine ni nzuri na itatusaidia sana kutokana na elimu ambayo imetolewa pale Bonyokwa wananchi wanakusanya taka na kuzigawa katika mafungu matatu kisha wanazilejeleza na zinazosalia wanazipeleka dampo" anasema

Mwenyekiti Ushirika wa Wakusanya Taka Bonyokwa, John Nsyenge, anayesema serikali inapaswa kuiga mfumo wanaoutumia na kuusambaza maeneo mengine ili kufikia adhima ya taka sifuri nchini.



Mkurugenzi wa taasisi ya usafi ya Nipe Fagio, Anna Rocha alipowasilisha mada katika mkutano unaomuhusu. **PICHA : HALFANI CHUSI.**

Anafafanua, mfumo wanaoutumia unajumuisha kupita majumbani na kutoa elimu ya kutenganisha taka katika makundi manne. Makundi hayo ni yale ya taka zinazooza, rejeshi, nyinginezo (zisizo na thamani) na hatarishi.

"Baada ya hapo nyingine tunazigeuza mbolea tunauza na tunapata kipato, tunatengeneza wadudu ambao ni chakula cha kuku na Samaki, pia imesaidia sisi kujiajiri tunapata fedha kutokana na makusanyo ya taka nyumba kwa nyumba" anasema mwenyekiti huyo huku akiomba serikali kuwaunga mkono

### HATUA SERIKALINI

Mkurugenzi Mkuu Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk Immaculate Semesi, anabainisha kuwapo kwa vikwazo katika kutekeleza mfumo wa taka sifuri na kwamba kinachosubiriwa ni tamko kutoka serikalini.

Anasema kazi yao ni kuelimisha na kutoa ushauri kwa Halmashauri na Wilaya husika kwa kushirikiana na Maofsa Mazingira katika usafi mazingira.

Anasisitiza kuwa mfumo wa Taka Sifuri unatija serikali inapaswa kuiga na kuutumia katika maeneo yote nchini ili wananchi wajue namna ya kugeuza taka kuwa fursa.

"Ni jukumu la serikali kuu na mamlaka husika, kutoa tamko kuhusu kutumia mfumo wa taka sifuri, tumeshafikisha maoni juu ya hilo sasa kilichobaki ni mamlaka kuweka nguvu katika hilo.

"Sisi ni wazalisha taka, lazima zirejelezwe ili kufikia taka sifuri ni uamuzi wa mamlaka za juu kutoa tamko halafu baada ya hapo sisi tutafuatilia na kuingia mtaani kutoa elimu kuhusu umuhimu wake.

"Tunatakiwa kuwa na gari angalau lenye sehemu mbili au zaidi ya kuweka taka zilizo tenganishwa nchi zilizo endelea zinafanya hivyo.

Mkurugenzi huyo anabainisha kuwa utaratibu huo ukitumika inawezekana kufikia adhima ya taka sifuri kwa asilimia 100. Immaculate anakemea kitendo cha watu binafsi kutupa taka ovyo akitamka:

"Ni kuuana na kuwekeana hatari katika masuala ya afya sisi tunakaulimbiu yetu inasema 'mazingira yetu tuyalinde tuyatunze anayeharibu mazingira kwa makusudi huyo ni muuaji'

Anaendelea na ufafanuzi wake kwamba Sheria ya mwaka 2004 inayotaka taka zitenganishwe kuanzia nyumbani ni butu na mtambuka kwamba ilifaa kila idara taasisi na sekta iwe na kipengele cha mazingira sheria mama ya mazingira inatoa mwongozo wa nini kifanyike lakini mwenye mamlaka ya kuchukua hatua ni sekta husika.





# Vijana watakiwa kuungana, kuacha kukaa vijiweni

Na Peter Mkwavila
DODOMA

KATIBU Tawala Msaidizi Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mkoa wa Dodoma, Mwajabu Nyamkomola, amesema kitendo cha vijana kukaa vijiweni bila ya kufanya kazi ni chanzo kikubwa cha kujiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya.

Nyamkomola alitoa kauli hiyo juzi wakati akifungua mafunzo kwa viongozi wa taasisi isiyo ya kiserikali ya Youth and Peace Development Economic Association (YPDEA) jijini hapa.

Alisema kitendo cha baadhi ya vijana kutumia dawa hizo, wamekuwa mzigo mkubwa kwa familia zao kuwalea na kwa serikali kwa kukosa nguvu kazi ya taifa.

Aliwataka vijana ambao hawana kazi kuungana, kuunda vikundi, kuanzisha miradi na kujiajiri.

Alisema fursa zipo nyingi ikiwemo za kilimo, ufugaji, uvuvi na kilimo cha bustani, kinachotakiwa kwa vijana hao ni kuchangamkia ili kupata mikopo inayotolewa na halmashauri nchini.

Rais wa YPDEA, Jeremia Musano, aliwataka viongozi, vijana na wanachama wa taasisi hiyo kuepuka vitendo vinavyokiuka sheria za nchini.

Musano, alisema endapo vijana wakiungana ndani ya taasisi hiyo na kuepukana na vitendo hivyo, wataisaidia serikali kuelimisha, kudumisha amani na utulivu.

Aliwataka wanachama wa taasisi hiyo kuepuka vitendo vya uvunjifu wa amani na kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan kuleta maendeleo nchini.

Aliwashauri kutofanya makosa kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa kwa kuchagua viongozi watakaomsaidia Rais Samia katika utendaji kwa manufaa ya Watanzania.

Awali Ofisa wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Kanda ya Kati, Anna Tengia, aliiomba YPDEA kushirikiana na serikali na jamii kudhibiti dawa za kulevya nchini.

# Jafo asisitiza wafanyakazi viwanda kufunga mkanda

Na Paul Mabeja, DODOMA

WAFANYAKAZI wa Wizara ya Viwanda na Biashara wamesisitizwa kufunga mkanda ili kuhakikisha sekta ya viwanda na biashara zinapiga hatua.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Selemani Jafo, hayo juzi baada ya kuripoti ofisini kwake tangu aapishwe kushika nafasi hiyo.

"Nimekuja tufanye kazi pamoja ili tumsaidie Rais, naomba ushirikiano kwani wizara ina mambo mengi na tuna kazi kubwa ya kufanya hasa katika masuala ya viwanda," alisema.

Alisema kwa sasa nchi ina wahitimu wengi na kuwa sekta hiyo ndio njia pekee ya kuhakikisha wanaingia kwenye soko la ajira au kujiajiri.

"Tuna kazi kubwa ya kufanya, nitawaomba tufunge mkanda kweli kweli katika eneo la viwanda," alisema.

Jafo ambaye aliteuliwa hivi karibuni na Rais Suluhu Hassan kushika wadhifa huo akitokea Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira.

Kwa upande wa sekta ya biashara, Dk. Jafo, alisema wanapaswa kuweka kipaumbele kwa kuhakikisha wanaweka mazingira mazuri ya ufanyaji biashara.

Alisema wakifanya hivyo, wataondoa tishio ya migomo kama iliyojitokeza hivi karibuni wafanyabiashara kutishia kufunga biashara katika mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza na Dodoma.

"Kwa upande wa biashara hii sehemu kwetu sisi tukilala tuwe tunafikiria biashara na hasa jinsi gani tutawasaidia eneo hili tufanye vizuri.

"Kwa mfano tumeshuhudia migogoro pale Kariakoo na tishio la migomo la wafanyabiashara, hivyo sisi tuna wajibu wa kuangalia jinsi gani tutaimarisha mazingira ya biashara, watu wakafanya biashara vizuri zaidi," alisema.

Alisema eneo lingine la kuweka mazingira ni kwa wafanyabiashara ndogo ndogo maarufu kama machinga na kusisitiza suala hilo atalitolea mwongozo ambao kipindi hicho kikifika, kila mtendaji lazima atekeleze aneo lake kwa weledi.

Pia aliwasisitiza watumishi kuacha kufanyakazi kwa mazoea, kuzingatia muda na kufanya kazi kwa weledi.

"Kila mtu ajipange kufanyakazi kwa kushirikiana, tujipange kuacha mazoea, tujipange kujali muda, tujipange kufanya kazi. Katika maisha yangu napenda watu wanaofanya kazi kila mmoja katika eneo lake."

Dk. Jafo pia aliagiza kukutana na wafanyakazi wote na menejimenti za taasisi zote 13 zilizochini ya wizara hiyo kuanzia wiki ijayo.

Awali, akimkaribisha, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Balozi John Simbachawene, alisema wizara inajukumu la kuleta maendeleo jumuishi na endelevu, kuchochea maendeleo ya sekta zilizochini yake na kulifikisha taifa katika kiwango cha uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda ifikapo mwaka 2025.

Alisema kwa sasa iko katika mchakato wa kufanyia marejeo sera, sheria na mikakati mbalimbali ili ziendane na wakati wa sasa katika sekta za viwanda na biashara.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo (katikati), akizungumza alipotembelea kiwanda cha mbolea cha Itracom Fertilizer Ltd jijini Dodoma juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Taasisi za umma zaagizwa kutumia NeST kwa manunuzi

Na Thobias Mwanakatwe, SINGIDA

KIONGOZI wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa kwa mwaka huu, Godfrey Mnzava, ameziagiza taasisi za umma kuzingatia Mfumo wa Ununuzi wa Umma (NeST ) wakati wa kufanya manunuzi ili kuweka uwazi na uwajibikaji.

Mnzava alisema hayo wakati akizungumza na wakazi wa Manispaa ya Singida jana baada ya Mwenge huo kukagua barabara ya Minga yenye urefu wa kilometa 1.21 iliyojengwa kwa kiwango cha lami kwa gharama ya Sh. 992,096,092.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameendelea kuelekeza manunuzi ya umma yapitie Nest ambao unasimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kuweka uwazi, uwajibikaji na kudhibiti manunuzi ya umma.

Alisema kupitia mfumo huo, wazabuni wanaomba zabuni moja kwa moja watajulikana nani mwenye sifa na nani hana sifa na kwamba huu ni mkakati wa serikali kuhakikisha kunakuwa na udhibiti katika manunuzi.

"Kumekuwa na malalamiko kuna watu wanapendelewa kupewa zabuni, lakini kupitia NeST hakuna cha upendeleo kwani unaona kitu gani umekikidhi na kipi haujakidhi," alisema Mnzava.

Kwa upande mwingine aliwapongeza Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) Manispaa ya Singida kwa kuzingatia mfumo huo kwa kuwa ni maelekezo ya serikali katika suala la manunuzi.

Awali Meneja wa TARURA wa Manispaa hiyo, Mhandisi Lazaro Kitomari, alisema barabara hiyo kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilometa 1.21 imejengwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ikiwa ni sehemu ya zinazotolewa kila mwaka kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

Mhandisi Kitomari, alisema TARURA ilipanga kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami katika awamu tatu, ya kwanza ilijenga kilometa 0.6 katika mwaka wa fedha 2021/22, ya pili kilometa 0.61 mwaka wa fedha 2022/23 na ya tatu mwaka wa fedha 2023/24 na kufunga taa barabarani 37.

Alisema gharama za mradi huo ni Sh. 344,128,092, awamu ya kwanza na Sh. 452,268,000 awamu ya pili mwaka wa fedha 2022/23.

Awamu ya tatu ambayo imetekelezwa na Mkandarasi OTONDE CONSTRUCTION & GENERAL SUPPLIES LTD wa Mwanza kwa Sh. 195,700,000 na hivyo ujenzi katika awamu zote tatu kufikia Sh. 992,096,092.

Aliongeza kuwa faida za barabara hiyo ni kupunguza gharama za uendeshaji vifaa vya usafiri, usafiri na usafirishaji, vumbi, uchafuzi wa mazingira, kupendezesha mji, kupunguza gharama ya ukarabati wa barabara mara kwa mara na kuongeza usalama wa watumia barabara.

Kauli mbiu ya Mwenge huo kwa mwaka huu ni "Uhifadhi wa Mazingira na uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Mkoani hapa unatarajiwa kuhitimisha mbio zake kesho kubwa na kukabidhiwa Manyara.





# Mradi mamilioni warudisha tabasamu kwa wananchi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Kata ya Mjela katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya mkoani hapa, wameondokana na adha ya kutembea umbali mrefu kutafuta maji baada ya serikali kukamilisha Mradi wa Maji wa Mshewe- Mjele.

Wakizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki iliyopita, wakazi hao walisema kabla ya mradi huo kukamilika walikuwa wanatumia muda mrefu kwenda kutafuta maji kwenye makorongo na kwenye mito, hali ambayo ilikuwa inasababisha washindwe kutekeleza baadhi ya majukumu.

Mmoja wa wakazi hao, Shupati Sinkwembe alisema walikuwa wanakwenda kuchota maji usiku kwenye makorongo ambako walikuwa wanakumbana na nyoka na wanyama wengine wakali wakiwemo fisi.

Sinkwemba, alisema kwa sasa maji yanapatikana kwa wingi katika eneo hilo na kwamba baadhi ya wakazi hao wenye uwezo wameingiza kwenye nyumba zao na hivyo tatizo la kupoteza muda kwenda kutafuta huduma hiyo limepungua.

Alisema uwepo wa huduma hiyo kumesaidia baadhi yao kuanza kujenga nyumba za kisasa kwa kuatumia maji hayo kufyatua tofali.

"Tunaishukuru sana serikali imetupunguzia tatizo hili la maji kwenye eneo hili, lakini bado halijamalizika maana kuna baadhi ya vitongoji vya pembezoni havijafikiwa na huduma," alisema Sinkwembe.

Alisema wakazi wa vitongoji hivyo wanalazimika kusafirisha maji hayo kwa kutumia pikipiki, punda na kubeba kichwani.

Upendo Emmanuel, alisema walikuwa wanapata shida zaidi kipindi cha kiangazi kutokana na maji ya kwenye makorongo kukauka`, hivyo kugombania kwenye visima vyenye chemchemi.

Alisema kutokana na eneo hilo kukabiliwa na ukame, serikali imelazimika kuchukua maji kutoka Kijiji cha Mshewe kilichopo umbali wa zaidi ya kilomita 20 hadi kijijini kwao.

Upendo, aliishukuru serikali kwa kutekeleza mradi huo na kuwaondolea adha ya muda mrefu ya kukosa maji.

Dereva wa bodaboda katika kata hiyo, Nijalie Gunza, alisema kuwepo kwa mradi huo, kumemuwezesha yeye na wenzake kupata ajira ya kupeleka maji kwa baadhi ya wakazi hao kila siku na kujipatia kipato .

Gunza, alisema baadhi ya wafugaji jamii ya Kimasai wanaoishi vitongoji ambavyo havijafikiwa na huduma hiyo, wanahitaji huduma hiyo na kumlipa kuanzia Sh. 2,000 mpaka 5,000 kwa siku.

Diwani wa Mjele, Tatizo Gunza, alisema kata yake ina vijiji vitatu vimeshaunganishiwa huduma hiyo ya maji na kuwapunguzia wakazi wake adha ya kukosa maji.

Alitaja sababu ya baadhi ya vitongoji kutounganishiwa huduma hiyo ni wakazi wake kuishi kwa kutawanyika hasa kutokana na wengi wao kuwa wafugaji ambao muda mwingi wako porini.

Mradi wa Maji wa Mshewe Mjele umetekelezwa na serikali kupitia Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) kwa garama ya zaidi ya Sh. bilioni mbili.



Mkurugenzi wa Shirika la Akili Platform Tanzania (APT), Roghat Robert, akichangia hoja katika kikao cha Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), mjini Tabora hivi karibuni. Tume hiyo inatarajia kuanza uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura kuanzia Julai 20, mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM waonyana upendeleo uchaguzi viongozi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe, kimewaonya viongozi wa matawi na kata kuacha upendeleo na kuwateua watu wanaokubalika kwa wananchi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika baadaye mwaka huu na Uchaguzi Mkuu 2025.

Katibu wa Siasa, Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa chama hicho Mkoa wa Njombe, Josaya Luoga, alitoa onyo hilo mwishoni mwa wiki iliyopita kwenye mkutano mkuu wa chama hicho Tawi la Mjimwema kwa lengo la kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Luoga, alisema wakati viongozi hao wakiwa wanapanga mikakati ya ushindi, lazima kuwaza kuwateua wagombea wanaokubalika zaidi na wananchi.

"Viongozi wangu wa matawi na kata, tunapokwenda kuteua wagombea tusiteue kwa upendeleo, tuwapate wagombea waadilifu, waaminifu, wakweli na wasiopewa mashaka yoyote na wananchi kwenye mitaa yetu, lakini wawe ni watu wanaokubalika," alisisitiza Luoga.

Awali akisoma taarifa ya utekelezaji, Katibu wa Tawi hilo, Emmanuel Mkane, alisema wamepata mafanikio ya ujenzi wa miradi, ikiwamo ofisi na kilimo cha miti kwa ajili ya kupandisha pato la tawi lao.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mjimwema, Lenard Mkupi alisema wanatekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo zikiwamo shule, zahanati na ofisi.

"Tayari wiki iliyopita tumepokea Sh. milioni 63 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mawili na matundu sita ya vyoo fedha hiyo imetoka kwenye mfuko wa boost," alisema Mkupi.

Diwani wa Viti Maalumu Tarafa ya Njombe Mjini, Angela Mwangeni, aliwataka wazazi kuwalinda watoto wao dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwemo ulawiti na ubakaji.

"Sasa hivi wanawake tumekuwa wazembe tunawaacha watoto wanafanyiwa vitendo vya hatari ambavyo ni vitendo vibaya, leo hizi shule tunazozisoma kama watoto wanafanyiwa vitendo vya ajabu hizi shule watakuja kusoma akina nani?" alihoji Mwangeni.

Baadhi ya wakazi wa Mtaa wa Mjimwema akiwemo Irene Makinda alisisitiza kuwa ni jukumu la kila mzazi na jamii kushiriki mapambano dhidi ya ulawiti, vipigo, ubakaji na utelekezaji watoto.

## Sekondari zakabidhiwa kompyuta

**Na Nebart Msokwa,** TUKUYU

SERIKALI imeikabidhi Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya kompyuta 10 za kufundishia somo la Habari ya Teknolojia na Mawasiliano (TEHAMA) kwa shule zake za sekondari za zilizoko maeneo ya pembezoni .

Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Maryprisca Mahundi alikabidhi kompyuta hizo mwishoni mwa wiki iliyopita kwa shule mbili na kuahidi kupeleka zingine kwa nyingine mbili zilizosalia hivi karibuni kulingana na upatikanaji wake.

Mahundi, alisema wizara hiyo imetoa kompyuta hizo kati ya 20 zilizoomba na Mbunge wa Rungwe, Anthony Mwantona kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na kuinua kiwango cha elimu kwa wanafunzi wa shule hizo nne.

Alisema kompyuta hizo ziliombwa kwa ajili ya Shule ya Sekondari Kisiba, Kisondela, Iponjola na Ikunga.

"Hizi kompyuta ni kwa ajili ya shule mbili ambazo kila moja itapatiwa tano na huu ni mwanzo tutaleta zingine 10 kwa ajili ya shule zilizobakia ili wanafunzi wetu wajifunze vizuri masomo haya ya kompyuta na wasiwe wageni watakapofika elimu ya juu," alisema Mahundi.

Hivyo, aliwataka walimu wa shule zitakazopatiwa kompyuta hizo kuhakikisha wanazitumia na kuzitunza vizuri ili zitumike kwa muda mrefu.

Akipokea kompyuta hizo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Renatus Mchau, alisema shule hizo zilipatiwa vifaa hivyo kutokana na kuwa mbali na maeneo ya mjini.

Katibu wa Mbunge wa Jimbo hilo, Gabriel Mwakagenda, alisema kompyuta hizo ni matokeo ya kikao kilichofanyika jijini Dodoma baina yao na Naibu Waziri huyo.

Kwa mujibu wa Mwakaganda, walipofanya ziara bungeni walionana na Naibu Waziri huyo na wakamuomba asaidie vifaa hivyo na kuahidi kuwapa na kwamba utekelezaji wake umeanza.



## Dk. Mwinyi mgeni rasmi mapambano ya rushwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, DK. Hussein Ali Mwinyi, anatarajia kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya Siku ya Mapambano ya Rushwa Afrika, yanayotarajia kufanyika katika viwanja vya biashara Nyamanzi Zanzibar.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alisema lengo kuu la maadhimisho hayo ni kutoa fursa kwa nchi wanachama kutafakari mafanikio na changamoto za utekelezaji na hatua zinazochukuliwa na wadau Afrika katika kuzuia na kupambana na rushwa.

Alisema tafakari hizo zinajikita katika kauli mbiu ya maadhimisho kwa mwaka husika na inasaidia kuweka mikakati endelevu ya kukabili tatizo la rushwa kupitia maoni na uzoefu wa wadau.

Alisema kauli mbiu ya mwaka huu ni 'Ulinzi wa mtoa taarifa, nyenzo muhimu katika mapambano dhidi ya Rushwa', inakwenda sambamba na nchi wanachama kuwapa ulinzi unaostahiki kwa wanaotoa taarifa za rushwa ili wasiweze kuathiriwa na watenda uovu baada ya kutekeleza wajibu wa kisheria.

Aidha, alisema kuwa vita ya rushwa ni kubwa kuliko vita ya silaha, hivyo ni jukumu la kila mmoja kuhakikisha wanazuia vitendo hivyo ambavyo vinadumaza maendeleo ya nchi.

Alisema kwa Zanzibar vitendo vya rushwa vimepungua kutokana na jitihada kubwa zinazochukuliwa na Rais Dk. Hussein Mwinyi hasa katika suala la kusimamia uwajibikaji.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), Ali Abdalla, alisema katika kuhakikisha wanafikia lengo la kuzuia rushwa nchini, wanaendelea na jitihada za kutoa elimu katika maeneo ya Unguja na Pemba.

Alisema lengo la kutoa elimu hiyo ni kuwashajiisha na kuwajengea uwelewa wananchi juu ya kuripoti vitendo vya rushwa katika maeneo yao.

# Viongozi CCM watakiwa kuacha kiburi, majivuno

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Hamad Hassan Chande, amewataka viongozi wa chama kutokuwa na majivuno wala kiburi wanapokuwa madarakani, kwani huo siyo utaratibu wa chama.

Alisema ni vyema viongozi wa chama hicho kuwa wanyenyekevu na ushirikiano kwa vijana ambao wameonesha nia ya kujiunga na chama.

Chande ambaye ni Mbunge wa Kojani aliyasema hayo katika tawi la CCM Kiuyu Kigongoni Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba alipofanya ziara ya kusikiliza kero na changamoto kutoka kwa wanachama wa chama hicho.

Aliwataka viongozi wa chama kuwalea vijana wanaoingia ndani ya CCM wawe tayari kukitumikia, kukilinda na kukiimarisha chama na mtaji wa ushindi na wanachama wengi.

Aidha, alifurahishwa na uamuzi wa vijana kujitokeza kwa wingi kujiunga na chama hicho na kuahidi kushirikiana nao katika kukiimarisha, sambamba na kuondoa changamoto zinazowakabili vijana hao.

Alisema atahakikisha anamaliza ujenzi wa tawi hilo sambamba na kuweka umeme ndani ya tawi hilo na amefurahishwa na hamasa iliopo kwa vijana hao.

Akizungumzia suala la ujenzi wa shule aliwahakikishia wananchi na wanachama wa CCM kwa ujumla kuwa amekusudia kujenga Shule ya ghorofa katika eneo la Kiuyu Kigongoni lenye madarasa 49.

Aidha, alisema kuna mpango wa kujengwa shule ya ufundi eneo la Kojani ili wanafunzi ambao hawakupata fursa ya kuendelea na masomo wapate elimu ya ufundi.

Katibu wa CCM Wilaya ya Wete Pemba, Said Nkindwa, alisema atahakikisha anashirikiana na mbunge huyo ili kuhakikisha chama kinaendelea kuongoza dola.

Alieleza kuwa ameanzisha madarasa sita ya itikadi ndani ya eneo la Kojani yenye wanachama 600 ambao kwa sasa wanahitaji kupatiwa kadi.

Katibu wa Siasa na Uenezi Wilaya ya Wete, Salim Omar Abdalla, alisema mbunge wa Kojani, Hamad Hassan Chande anafanya kazi kubwa na imara ya kutekeleza ilani ya chama.



Ofisa Mifugo, Rose Wambura, akitoa chanjo kwa mbwa wakati wa maadhimisho ya siku ya kimataifa ya magonjwa ya Zuonotiki Duniani, mkoani Mara hivi karibuni. Ili kupambana na magonjwa haya, serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu ilizindua kampeni ya kitaifa iitwayo 'Holela Holela Itakukosti' inayotekelezwa kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), kupitia mradi wa Breakthrough ACTION. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NGOs zatakiwa kushirikiana na serikali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wamezitaka asasi za kiraia kufanya kazi kwa karibu na serikali kwa ajili ya kuharakisha maendeleo na kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili wananchi.

Wito huo umetolewa na mwakilishi wa Pandani, Profesa Omar Faki Hamad wakati akizungumza na viongozi wa asasi za kiraia wakiongozwa na Jumuiya ya Wanawake wenye Ulemavu (JUWAUZA).

Alisema asasi za kiraia zina nafasi kubwa katika kuiokoa nchi kwenye mambo tofauti ikiwamo mambo shirikishi bila ya ubaguzi na kwamba kuna uhusiano mkubwa kati ya asasi za kiraia na taasisi za kiserikali.

Alisema ili juhudi za watu wenye ulemavu kufanikiwa serikali inapaswa kuziona jumuiya za watu wenye ulemavu ni washiriki badala ya washindani na kuiokoa nchi katika mambo tofauti.

"Ni lazima watu wenye ulemavu kupitia jumuiya zao kuwa shirikishi katika utekelezaji wa miradi bila ya ubaguzi bila ya kujali ulemavu wao," alisema.

Alisema semina hiyo itasaidia hasa makatibu wa kamati za Baraza la Wawakilishi kuelewa kuna uhusiano mkubwa kati ya asasi za kiraia na taasisi za serikali katika kushirikiana kutekeleza baadhi ya mambo wanayoyahitajika.

Alisema kuna changamoto za kisheria na kusababisha kupunguza nguvu za kufanya kazi asasi za kiraia ikiwamo za watu wenye ulemavu, hivyo semina hiyo itawasaidia kutunga sheria kwa kuzingatia mambo yanayokwaza jumuiya hasa asasi za kiraia.

Aidha, alisema ushirikishwaji wa raia katika utekelezaji wa haki na wajibu wa watu wenye ulemavu unapatikana kwa mujibu wa sheria na pale sheria zinapokwaza kurekebishwa ili haki ya msingi kupatikana.

Mwakilishi wa Malindi, Mohamed Ahmada Salum, aliwataka watendaji wa asasi za kiraia kufuatilia kwa karibu mambo mengi yanayofanyika katika Baraza la Wawakilishi ikiwamo vikao pamoja na miswada ya sheria ili kuona kwa kiasi gani mabadiliko yake yanawagusa.

Katibu wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi, Othman Haji, alisema katika utaratibu wa Baraza la Wawakilishi asasi za kiraia zinaruhusiwa, kwamba zinakaribishwa kwa ajili ya kusaidia na kutoa maoni katika mwenendo wa bajeti na shughuli nyingine.

"Hakuna sheria zinazowabana asasi za kiraia katika utekelezaji wa majukumu yao na kufanya kazi na Baraza la Wawakilishi... umuhimu wa asasi za kiraia upo wazi unafahamika, ni sehemu ya uwakilishi wa wananchi," alisema.

Akiwasilisha mada kuhusu mradi wa uraia wetu unaotekelezwa na JUWAUZA kwa ufadhili wa Jumuiya ya Ulaya (EU), mratibu wa mradi huo, Suleiman Baitani, alitaka ushirikiano na muhimu wa Baraza la Wawakilishi ambao sehemu ya majukumu yake ni kutunga sheria za nchi.

Mwenyekiti wa JUWAUZA, Salma Sadatti, aliipongeza serikali katika Bajeti Kuu ya Mwaka 2024-2025 kwa kuondoa ushuru wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa vifaa vinavyotumiwa na watu wenye ulemavu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**LINDA NURU MATHEW KEA** anatangaza kupotea kwa cheti cha chuo na transcript ya **BACHELOR OF ARTS IN PUBLIC REKATION AND ADVERTISING** vyenye usajili namba 2017-04-11803 vilivyotolewa na **CHUO CHA UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM** mwaka 2020. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/23356/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**AMOS KAMUGISHA AUGUSTINE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1457-0019** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ATIBANDA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2010. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/UBU/139893/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**HAMZA JUMA MUSSA** anatangaza kupotea kwa cheti cha chuo cha **BACHELOR OF ACCOUNTING** chenye registration number **IMC/BAC/18/97693** kilichotolewa na **INSTITUTE OF FINANCE MANAGEMENT MWAKA 2021** kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochte cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/114180/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**FREDERICK D. SAGAMIKO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S137/0861** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MKWAWA SEKONDARI mwaka 1999. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **IF/RB/2216/2013.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SWED ATHUMANI KISOKILE**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya SCANIA yenye usajili namba **T 935 EFX** na CHASSIS NAMBA: **Y5R6X200005471881** na TRAILER yenye usajili namba: **T 761 EFU.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/DAR/KIG/101692/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HAMADI OMARI MNGOMA**

anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **FEKON** yenye usajili namba **MC 780 DEZ.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/TAN/MUH/6684/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SHARIFA AHMED SIJAONA**

anatangaza kupotea kwa akdi ya gari aina ya **TOYOTA MARK TWO GRAND** yenye usajili namba **T 537 BJE .** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/DOD/DOD/9519/2023**

### DEED POLL

**(Made under the registration of documents ordinance [CAP 117])**

**BY THIS DEED,** I the undersigned **SHABANI AHMED KANIKI** a citizen of the united republic of Tanzania by birth to hereby state;

1. **THAT,** for and on behalf of myself, wish to **CONFIRM** the use of the three names – **SHABANI AHMED KANIKI** which have been in use from the date of my birth and that these names are and I will continue to be in use for the rest of my life, unless and until decided otherwise, in all records, deeds, transactions and writings in all occasions whatsoever, and;
2. **THAT,** I renounce, abandon and relinquish the names **SHABANI AHMED** which have been used in some of the past records, deeds, documents, transactions.

**IN WITNESS WHEREFORE,** I do hereby confirm and declare that my names are and shall continue to be **SHABANI AHMED KANIKI.**

SIGNED and DELIVERED by the said SHABANI AHMED KANIKI who is known to me personally this 28 day of June 2023



DEPONENT

Name: ALLY Y. MAKAMBA

Signature:

Postal Address: P.O. Box 7575 DAR ES SALAAM

Qualification: COMMISSIONER FOR OATHS

### IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 14846/ 2024**

**In the matter of the Estate of the late TITUS KAZONI PESHA**

**AND**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY BENTA ROBERT KAKASEKO and GLADNESS TITUS PESHA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before the 25 Day of JULY, 2024

Dated at Dodoma this 9 Day of JULY, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SHEDRACK THOBIAS MNZAVA**

anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki aina ya King Lion yenye namba za usajili **MC 237DJH,** Chasis namba ***LZL15P900MHL46083*** na Engine namba **KL162FMJ*211146083***

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

TAARIFA YA POLISI:

**BAB/TR/RB/272/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FESTO RICHARD SANGA**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T524DVF** aina ya **TRAILER,** Chassis No. **C207310,** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya Polisi:

**PHQ/DOD/DOD/28847/2024**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail:**
**advertise@guardian.co.tz,**
**website:**
**www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Viongozi wa NATO wakutana Marekani

**WASHINGTON,** Marekani

VIONGOZI wanaounda Jumuiya ya Kujihami ya NATO, jana wameanza mkutano wao nchini Marekani, ajenda kuu ni kuiunga mkono Ukraine.

Hata hivyo, viongozi watazungumzia jinsi ya kuimarisha umoja wao kutokana na changamoto zinazozikabili nchi za Ulaya.

Kabla ya mkutano huo, kulitanguliwa na sherehe za kuadhimisha miaka 75 tangu kuanzishwa kwa muungano huo wa kijeshi, zilizofanyika usiku wa kuamkia jana katika jiji la Washington.

Rais wa Marekani, Joe Biden ambaye ndiye mwenyeji wa mkutano huo anatazamiwa kuhimiza mshikamano na ushirikiano kwa nchi wanachama pamoja na kuwahakikishia wapigakura wa Marekani kwamba bado ana uwezo wa kuongoza kwa muhula wa pili.

Katika moja ya ajenda kwenye mkutano huo ni kujadili mpango wa Katibu Mkuu wa NATO anayemaliza muda wake, Jens Stoltenberg, wa kuipatia Ukraine msaada wa kijeshi wenye thamani ya euro bilioni 40, ifikapo mwaka 2025.

Stoltenberg alisema matokeo ya vita dhidi ya Russia yatatoa mwelekeo wa usalama wa kimataifa kwa miongo kadhaa ijayo. Kulingana na Stoltenberg, NATO inahitaji kuishawishi Russia kwamba haiwezi kushinda vita vyake dhidi ya Ukraine.

"Ukweli ni kwamba hakuna njia mbadala isio na gharama kwa uchokozi wa Russia kama jirani. Hakuna njia isiyo ya hatari katika vita. Na kumbuka, gharama kubwa na hatari kubwa zaidi itakuwa kuiacha Russia kuishinda Ukraine. Hatuwezi kuruhusu hilo litokee," alisema Stoltenberg.

Kiongozi huyo wa NATO alisisitiza kuwa muda wa kusimama imara kwa ajili ya uhuru na demokrasia ni sasa. Wanachama wa NATO wameiunga mkono Ukraine, tangu Russia ilipoivamia nchi hiyo Februari mwaka 2022.

Wakati akizindua mkutano huo juzi, Rais Biden alisema washirika wa NATO watatoa mifumo zaidi ya ulinzi wa anga kwa Ukraine.

Hata hivyo, Rais wa Ukraine, Volodomyr Zelensky, ambaye anahudhuria mkutano huo, ana matumaini kwamba mkutano wa viongozi 32 kutoka nchi wanachama wa NATO utafafanua matarajio ya nchi yake.

Viongozi hao pita wanategemewa kujadili changamoto zinazosababishwa na China kutokana na kutoa msaada wa vifaa vya kivita kwa Russia.

Viongozi wa Australia, Japan, New Zealand na Korea Kusini, ni miongoni mwa wale walioalikwa kuhudhuria mkutano huo.

***DW***



Raia wa Ukanda wa Gaza wakitafuta manusura baada ya vikosi vya Israel kushambulia majengo kadhaa katika eneo hilo juzi.
**PICHA: GETTY IMAGES**

# Wengine 29 wauawa Gaza

**GAZA,** Palestina

WATU 29 wameuawa baada ya shule nyingine iliyoko kusini mwa Ukanda wa Gaza kushambuliwa na jeshi la Israel jana.

Tukio hilo limetokea siku nne baada ya shule nyingine kushambuliwa kwa makombora na kuwaua watu kadhaa katika mfululizo wa mashambulizi ya anga katika eneo hilo.

Hata hivyo, kundi la Hamas limelaani mashambulizi hayo na kuilaumu Israel kwa kuwaua watu kwa makusudi.

Jeshi la Israel lilisema linachunguza taarifa za shambulio hilo jipya.

Chanzo katika hospitali ya Nasser iliyoko Khan Younis kimeliambia shirika la habari la AFP kwamba shambulio hilo lililolenga mlango wa shule ya Al-Awda ambayo iko Abassan, mashariki mwa mji huo na kusababisha vifo vya watu hao.

Kwa upande wake, ofisi ya habari ya Hamas imeshutumu mauaji hayo iliyoeleza kuwa ya kutisha.

"Mauaji haya ni mwendelezo wa mauaji ya halaiki ambayo jeshi linalokaliwa kwa mabavu limeanzisha dhidi ya watu wetu wa Palestina kwa mwezi wa kumi mfululizo," ilisema taarifa hiyo ya Hamas.

Kabla ya shambulio hilo, shule tatu zinazohifadhi watu waliokimbia makazi yao zilikumbwa na mashambulizi ya Israeli tangu Jumamosi na kusababisha vifo vya takriban watu 20. Wakati huo huo, Rais wa Misri Abdel Fattah al Sisi na Mkurugenzi wa Shirika la Ujasusi la Marekani CIA, William Burns, walimejadili kuhusu juhudi za kufikia usitishaji mapigano Ukanda wa Gaza.

Ofisi ya Rais wa Misri ilieleza kwamba Al Sisi alithibitisha msimamo wa nchi yake wa kupinga operesheni ya kijeshi inayoendelea Ukanda wa Gaza.

Hata hivyo taarifa zilisema mazungumzo ya kutafuta amani yanayofanyika mji wa Doha yataanza tena kesho Jumatano na baadaye kuhamishiwa nchini Misri.

***RFI***

## Nchi ya Kenya haikopesheki

**NAIROBI,** Kenya

KENYA imetajwa kuwa miongoni mwa nchi ambazo zimevuka mstari mwekundu na haiwezi kukopesheka kutokana na kuelemewa na idadi kubwa ya madeni.

Nchi hiyo ina deni la dola bilioni 80 kutoka kwa mashirika ya kifedha kama Benki ya Dunia, Shirika la Fedha Duniani (IMF) na China.

Kulingana taarifa ya taasisi ya kimataifa ya kutathmini viwango vya ukopeshaji inayoitwa Moody, iliishusha Kenya katika nchi zenye deni himilivu na kuiorodhesha katika viwango vya chini zaidi ambavyo haiwezi kukopesheka.

Taasisi hiyo ilitahadharisha kwamba hali ya taifa hilo ni mbaya, baada ya wimbi la maandamano kumlazimisha Rais William Ruto, kukataa kusaini muswada wa fedha wa 2024, ambao uliongeza wigo wa kodi.

Taasisi hiyo yenye makao yake nchini Marekani, ilisema imeteremsha viwango vya uwezo wa Kenya kukopa kwa hatua moja chini, hali ambayo inatazamwa tishio kwa nchi hiyo ya Afrika Mashariki kuhusiana na uwezo wa kupata mkopo.

Tathmini hiyo mpya ya Taasisi ya Moody huenda ikaitumbukiza Kenya katika mgogoro wa kifedha kutokana na na gharama kubwa ya ulipiaji madeni yake.

Mchambuzi wa uchumi kutoka nchini humo, Mbui Wagacha, ambaye alikuwa mshauri wa zamani wa Rais mstaafu wa Kenya, Uhuru Kenyatta, alisema iwapo nchi hiyo itakopa zaidi, basi hilo ni jambo linaloweza kuitumbukiza katika matatizo zaidi.

Wagacha alipendekeza mkakati wa kutumia diplomasia kwa ajili ya kuvutia uwekezaji na kuliangalia upya deni la nchi hiyo ili kuwashawishi wakopeshaji walifute.

***DW***



## Waja na Marathon kuchangisha fedha

**Na Christina Mwakangale**

CHUO cha Uhasibu Tanzania (TIA) kimeandaa mbio za marathon kwa ajili ya kuchangisha fedha za kutunisha mfuko wa kuwalipia ada wanafunzi wenye mahitaji maalumu wakiwamo watu wenye ulemavu.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TIA, William Pallangyo, alisema hayo jana akizungumza na waandishi wa habari katika Banda la TIA kwenye Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba na yatazinduliwa hivi karibuni na Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba.

Alisema taasisi hiyo imebaini kwamba wapo wanafunzi ambao wanafanya vizuri katika masomo, huku baadhi yao wakishindwa kumudu gharama za masomo.

"Tunaandaa 'TIA Marathon' ambazo zitafanyika Oktoba 26, mwaka huu na tutafanya ufunguzi rasmi mwezi huu, sehemu ya pesa itakayopatikana itawasaidia wanafunzi wetu ambao tangu shule ya msingi walipata fursa ya kusoma hadi sekondari kwa ufadhili wa serikali, lakini kwa sasa wanakwama huku juu.

"Tunalenga kuunga mkono serikali kwa namna inavyosaidia vijana kupata elimu, kuwasaidia ambao hawana uwezo wa kulipa ada, kununua vifaa maalum vya kujifunzia kwa wale wenye mahitaji maalum.

**"Lakini kuna kundi ambalo wanafunzi wameanzisha familia ila hawana uwezo wa kusoma, awe na mlezi wa mtoto na amlipe. Tunatarajia mbio hizi zitafunguliwa na Waziri wa Fedha na Mipango na zitakuwa mbio za kilomita tano, 10 na 21."**

Aidha, Pallangyo alisema taasisi hiyo inaandaa kongamano la tatu la Kimataifa jijini Arusha, Novemba mwaka huu litakalofunguliwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dotto Biteko na kuhudhuriwa na nchi tofauti.

# WAZIRI MKUU AITAKA MTIBWA LIGI KUU BARA

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amembebesha 'zigo' Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, kuhakikisha anafanya kila jitihada ya kuirejesha Ligi Kuu msimu ujao klabu ya Mtibwa Sugar.

Mtibwa Sugar ilishindwa kuhimili ligi hiyo msimu uliopita na kujikuta ikishuka daraja baada ya kumaliza ligi kwenye nafasi ya mwisho.

Waziri Mkuu Majaliwa alisema hayo jana wakati akizindua tawi la benki moja mkoani hapa.

" Morogoro mkoa wa michezo, hivi Mkuu wa Mkoa Malima, Mtibwa ipo? sasa Benki imekuja nafiriki Mtibwa sasa itarudi tu", alisema Majaliwa.

Aidha, alisema kuwa Mtibwa Sugar ni Chuo cha Wanamichezo katika mpira wa miguu hapa nchini.

" Wafadhili wamekuja, RC (Mkuu wa Mkoa) irudishe Mtibwa kwenye ligi kuu, wadhamini wapo, ianze kwanza na ligi daraja la kwanza ili Mtibwa irudi ligi kuu na harafu iendelee nayo," alisema Majaliwa.

Mkurugenzi wa benki hiyo iliyozinduliwa tawi lake mkoani hapa, Arafat Ally Haji mbali na wadhifa huo pia ni Makamu wa Rais wa klabu ya Yanga.

Mtibwa Sugar iliwahi kutwaa ubingwa Tanzania Bara mwaka 1999 na 2000 wakati huo ikiwa chini ya Kocha John Simkoko.



Mshambuliaji wa Singida Black Stars, Edmund John (kulia), akijaribu kumtoka beki wa APR wa Rwanda kwenye mchezo wao wa Kombe la Kagame juzi uwanja wa KMC, Dar es Salaam, Singida walifungwa bao 1-0. **PICHA: BINZUBEIRY**

# AZAM YAFUATA MAKALI ZANZIBAR

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Azam FC, kimetua mjini Zanzibar na tayari kimeanza kambi kujiandaa na Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika watakayoshiriki baada ya kupita miaka 10.

Kikosi cha wachezaji wa timu hiyo na benchi la ufundi kilitua juzi na jana kilianza mazoezi ambayo yanaweza kuendelea kwa siku kadhaa kabla ya safari ya kwenda nchini Morocco.

Mkuu wa Idara wa Habari wa Klabu hiyo, Thabit Zakaria 'Zaka', alisema wachezaji walianza kuwasili tangu Julai Mosi na wamekwenda Zanzibar kwa muda, wakati wakijiandaa na safari ya kwenda nchini humo kwa ajili ya kuendelea na 'pre season' ili kuwaandaa wachezaji kwa msimu ujao.

"Tunategemea kurejea Dar es Salaam kuanzia Julai 14 , halafu tutaondoka kwenda nchini Morocco kuweka kambi ndefu sasa na hiyo ndiyo 'pre season' yetu kwa msimu huu, tutakaa huko hadi mwishoni mwa mwezi huu ndipo tutakaporejea tayari kwa kuanza msimu mpya wa mashindano," alisema.

"Tutakuwa kule (Morocco) mpaka mwishoni mwa mwezi Julai tutarejea nchini kuja kumalizia maandalizi ya mwisho kabla ya kufungua msimu rasmi kwa mechi za Ngao ya Jamii, nadhani hapo kila kitu kitakuwa kiko tayari kwa Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo tunaipa kipaumbele kwani ni muda mrefu hatujashiriki," alisema Zaka.

Wakati Azam ikitarajiwa kwenda Morocco, tayari Simba imeshakwenda nchini Misri kuweka kambi, huku Yanga ikitarajiwa kuelekea Afrika Kusini kwa ajili ya mechi ya 'Toyota Cup' dhidi ya Kaizer Chiefs itakayochezwa Julai 28 kwenye uwanja wa Bloemfontein.

## ZISIKUPITE

### ZIRKZEE 'FRESH' MAN UNITED

KLABU ya Manchester United imekubaliana maslahi binafsi na mshambuliaji wa Uholanzi, Joshua Zirkzee na wako kwenye mazungumzo na Bologna kuhusu jinsi klabu hiyo ya Italia inataka kima cha kuachiliwa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(CaughtOffside)***

### LUKAKU, CASARE KUTOLEWA

CHELSEA iko tayari kuwatoa mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 31 na kiungo wa kati wa Italia, Cesare Casadei mwenye umri wa miaka 21 kwa Napoli ili kusaidia kupunguza bei ya mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 25. ***(Teamtalk)***

### ARSENAL BADO KWA CALAFIORI

ARSENAL bado haijafikia bei ya Bologna ya pauni milioni 42.3 kwa ajili ya kumnunua mlinzi wa Italia, Riccardo Calafiori mwenye umri wa miaka 22, mazungumzo kati ya klabu hizo mbili yanaendelea. ***(Football Italia)***

### ROYAL ATAKIWA AC MILAN

AC Milan imetoa ofa ya awali kwa beki wa kulia wa Tottenham Hotspur na Brazil, Emerson Royal lakini kuna pengo kati ya tathmini ya klabu kuhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Sky Sports Italia)***

### GROSS HUYO DORTMUND

KIUNGO wa kati wa Ujerumani, Pascal Gross amekubali maslahi binafsi na Borussia Dortmund, ambao wako kwenye mazungumzo ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 kutoka Brighton kwa kati ya pauni milioni 6. ***(Sky Sports Germany)***

### GALLAGHER ATAKIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur imehusishwa na kiungo wa kati wa Chelsea, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 24, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa England hana uwezekano wa kuhamia Spurs msimu huu wa joto.***(Football Insider)***

### MIGUEL ALMIRON KUUZWA

WINGA wa Newcastle United, Miguel Almiron yuko kwenye mazungumzo na mwakilishi wake kuhusu mustakabali wake huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Paraguay mwenye umri wa miaka 30 akihusishwa kutaka kuhamia Saudi Arabia na Magpies wanaaminika kuwa tayari kumuuza. ***(Chronicle)***

### MORATA ATAFAKARI HATIMA YAKE

MSHAMBULIAJI wa Hispania, Alvaro Morata, anatafakari iwapo ataondoka Atletico Madrid na kujiunga na AC Milan huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 akisema atasalia katika klabu hiyo ya Hispania hadi ashinde nao kitu. ***(Corriere dello Sport)***

### WIRTZ AGOMBEWA

REAL Madrid ina imani kuwa inaweza kuwashinda wapinzani wao Barcelona katika mbio za kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Bayer Leverkusen na Ujerumani, Florian Wirtz mwenye umri wa miaka 21. ***(Sport)***

### MARTINEZ ALIKARIBIA MAN UTD

WAKALA wa mlinda mlango wa Argentina, Emiliano Martinez mwenye umri wa miaka 31 amesema Manchester United ilikuwa karibu kumsajili kutoka Aston Villa msimu uliopita wa majira ya joto lakini Kocha Erik ten Hag aliamua kumnunua Andre Onana wa Cameroon mwenye umri wa miaka 28 badala yake. ***(ESPN)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# MEYA AMKATAA GREENWOOD MARSEILLE

**Kiongozi huyo amezungumzia tabia ya nyota huyo wa Manchester United kuwa isiyoelezeka kutokana na...**

**MARSEILLE,** UFARANSA

MEYA wa Jiji la Marseille ameiambia Olympique de Marseille kutomsajili Mason Greenwood wa Manchester United, akiitaja tabia ya fowadi huyo kuwa "isiyoelezeka," baada ya vyanzo kuiambia ESPN klabu hizo mbili kufikia makubaliano juu ya uhamisho wa kudumu wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22.

Greenwood alitumia msimu uliopita kwa mkopo Getafe. Hajaichezea United tangu kusimamishwa na klabu hiyo Januari 2022 baada ya kukamatwa kwa tuhuma za ubakaji na unyanyasaji, huku Polisi wa Greater Manchester wakithibitisha kuwapo kwa „picha na video za mitandao ya kijamii zilizotumwa na mwanamke akiripoti matukio ya ukatili wa kimwili."

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England alishtakiwa kwa jaribio la ubakaji, kujihusisha na tabia ya kulazimisha ngono na shambulio lililosababisha madhara halisi ya mwili, ingawa mashtaka yalifutwa baadaye.

"Tabia ya Greenwood haielezeki, haikubaliki," alisema Meya wa Marseille, Benoît Payan akikiiambia kituo cha redio cha Ufaransa RMC siku ya Jumanne.

„Kumpiga mkewe, niliona picha ambazo zilinishtua sana na hawezi kuwa na nafasi yake kwenye timu hii.

"Maadili ya OM na Marseille si chochote lakini kwa kweli. Ni aibu. Nitamwomba Rais wa Marseille, Pablo Longoria asimsajili Greenwood. Sitaki klabu yangu kufunikwa na aibu ya mtu ambaye anampiga mkewe."

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Marseille wamekubali kufanya makubaliano yenye thamani ya pauni milioni 26.7 pamoja ikijumuisha nyongeza pamoja na kifungu kikubwa cha mauzo, ili kumsaini Greenwood.

Katika mkutano na wanahabari siku ya Jumanne, Kocha wa Marseille, Roberto De Zerbi, alisema hatashikilia chuki dhidi ya Greenwood kwa sababu ya maisha yake ya zamani.

"Mason ni mchezaji wa kiwango cha kimataifa, lakini bado hatujamsajili, sijui nini kilitokea, lakini sijazoea kujihusisha na maisha ya binafsi ya wachezaji wangu. Lakini akija hapa lazima ujue kwamba ninawatendea wachezaji wangu wote kama wanangu naweza kuwasema kwa faragha, lakini siwezi kuwashambulia hadharani."

# YAMAL AWEKA REKODI HISPANIA IKITINGA FAINALI EURO

**MUNICH,** UJERUMANI

KOCHA wa Hispania, Luis de la Fuente alisifu "fikra" ya Lamine Yamal baada ya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kufunga katika michuano ya Ulaya kwa wanaume siku ya Jumanne alipofunga bao katika ushindi wa 2-1 dhidi ya Ufaransa.

Yamal mwenye umri wa miaka 16, alisawazisha bao la ufunguzi la Randal Kolo Muani kwa mkwaju wa ajabu wa dakika ya 21 ukimpita kipa wa Ufaransa, Mike Maignan.

Dani Olmo aliiongezea Hispania bao la pili dakika nne baadaye kukamilisha mchezo huo na kutinga fainali mjini Berlin watakayocheza dhidi ya England au Uholanzi Jumapili.

"Tumeona uwezo wake na fikra," alisema De la Fuente katika mkutano na waandishi wa habari.

"Ni mchezaji ambaye tunapaswa kumtunza, lazima nimpe ushauri wa kuendelea kufanya kazi kwa unyenyekevu sawa na kuweka miguu yake sakafuni.

"Ataendelea kukua, lakini ukomavu na mtazamo wake katika umri mdogo tayari ni kama ule wa mchezaji mwenye uzoefu zaidi. Tuna bahati kuwa ni Mhispania na tunaweza kumfurahia kwa miaka mingi zaidi."

Bao la kwanza la Yamal katika michuano hiyo pia ana pasi tatu za mabao, lilimfanya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kufunga kwenye Euro za wanaume akiwa na umri wa miaka 16 na siku 362.

Mfungaji mdogo zaidi wa awali alikuwa mchezaji wa Uswisi, Johan Vonlanthen (miaka 18, siku 141), alipocheza pia dhidi ya Ufaransa, kwenye Euro 2004.

Ilikuwa rekodi ya pili muhimu iliyowekwa kwenye fainali hizo na chipukizi huyo wa Barcelona, ambaye tayari alikuwa kijana mdogo zaidi kushiriki katika michuano ya Euro akiwa na umri wa miaka 16 na siku 338 alipoingia uwanjani katika mchezo wa ushindi kwenye Kundi B dhidi ya Croatia.

"Nimefurahi kwamba tuko kwenye fainali, lakini bado hatujafanya jambo muhimu zaidi, ambalo ni kushinda," alisema Yamal, ambaye atatimiza miaka 17 Jumamosi.

"Tulikuwa katika wakati mgumu nilipofunga, hatukutarajia kufungwa hivi karibuni. Nilikuwa nikilenga kona ya juu kabisa ambapo shuti langu liliende na ilikuwa ni hisia tu ya furaha.

"Najaribu kutofikiria sana kile kinachoendelea, nataka tu kujifurahisha na kusaidia timu. Nilikuja hapa kushinda mechi zote ili niweze kusherehekea siku yangu ya kuzaliwa hapa Ujerumani na wachezaji wenzangu wote."

Yamal pia alionekana kumjibu kiungo wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot, ambaye alisema kabla ya mchezo kijana huyo angelazimika kufanya zaidi ya alivyofanya hadi sasa kwenye Euro 2024 ikiwa angetaka kufika fainali.



## Mbappé: Sikuwa na bahati Euro hii

**MUNICH,** UJERUMANI

KYLIAN Mbappé alikubali kampeni yake ya Euro 2024 haikufaulu kwake baada ya Ufaransa kufungwa mabao 2-1 juzi Jumanne kwenye nusu fainali dhidi ya Hispania kwenye Uwanja wa Allianz Arena.

Mbappé alitoa asisti kwa Randal Kolo Muani na kuipa Ufaransa uongozi wa mapema mjini Munich, lakini Hispania ilijibu kupitia kwa Lamine Yamal na Dani Olmo na kutinga fainali watakayocheza dhidi ya dhidi ya England au Uholanzi mjini Berlin Jumapili.

Fowadi huyo wa Real Madrid amefunga bao moja pekee kwa penalti dhidi ya Poland katika hatua ya makundi katika mechi tano.

„Ushindani wangu? Ulikuwa mgumu," alisema Mbappé akiwaambia waandishi wa habari.

„Ilikuwa ni kushindwa. Tulikuwa na nia ya kuwa mabingwa wa Ulaya, nilikuwa na nia ya kuwa bingwa wa Ulaya, lakini tumeshindwa.

„Ni mpira wa miguu, tunapaswa kusonga mbele lakini umekuwa mwaka mrefu. Nitaenda likizo na kupumzika, hiyo itanisaidia sana na nitajaribu kurudi kwa nguvu. „

Michuano hiyo kwa Mbappé ilianza kwa njia mbaya zaidi wakati alipovunjika pua kwenye mchezo wa ufunguzi wa Ufaransa dhidi ya Austria.

Hilo lilimlazimu kukosa mchezo dhidi ya Uholanzi, lakini alirejea akiwa amevalia maski dhidi ya Poland, Ubelgiji na Ureno.

## Messi atinga fainali Copa America

**NEW JERSEY,** MAREKANI

LIONEL Messi alisema aliachwa na mshangao baada ya Argentina kuifunga Canada 2-0 kwenye Uwanja wa MetLife huko East Rutherford, New Jersey na kufuzu kwa fainali ya Copa América 2024.

Messi alifunga bao lake la kwanza kwenye Copa mwaka huu na la 14 la maisha yake katika kipindi cha pili baada ya Julian Álvarez kuifungia Argentina kwa bao lake la kipindi cha kwanza.

"Hii timu imefanya nini, timu ya taifa ya Argentina imefanya nini, kwa sababu baada ya hii kila mtu anatoa umuhimu zaidi kwa fainali zote ambazo mimi na wenzangu tumecheza," alisema Messi baada ya mechi.

"Mimi, Fide (Angel Di María), Ota (Nicolás Otamendi), na kwamba Argentina inaweza kucheza fainali nyingine ni ajabu.

"Kusema kweli yamekuwa mashindano magumu, kiwango kimekuwa sawa kama zamani, joto la juu ambalo hufanya iwe ngumu kucheza, wapinzani wagumu sana. Kwa hiyo ukweli tulifanikiwa na tuko hapa tena."


La Albiceleste inarejea kwenye mchezo wa fainali ya michuano hiyo kwa mara ya pili mfululizo, baada ya kushiriki mwaka 2021, na iko kwenye ukingo wa kushinda taji la 16 la Copa América nchini humo ambalo litawavuta mbele ya Uruguay kwa kushinda mara nyingi.

Kocha Lionel Scaloni alionesha kufurahishwa na kufikia hatua hiyo, kabla ya kuonya juu ya ugumu unaokuja kwa Argentina.

"Ni jambo la kujivunia na kushukuru kwa wachezaji," aliseema Scaloni.

"Mwenzangu aliniuliza kama tunarekebisha hili, lakini swali lilikuwa zuri na sikueleweka, ni ngumu sana kuingia fainali, haswa kuja kwa jinsi tulivyofanikiwa na ushindi.

"Walio ndani wanajua jinsi ilivyo vigumu kufikia hatua hii. Ni hisia za furaha, lakini pia wasiwasi kwa sababu inagharimu zaidi."



Argentina iliongoza Kundi A kwa kuzishinda Canada, Chile na Peru, kabla ya kwenda kuifunga Ecuador katika hatua ya mtoano na kutinga nusu fainali.

Messi na wenzake waliipeleka Canada katika nusu fainali kwa alama sawa na ilivyokuwa katika mchezo wa kundi wakishinda 2-0 na kuipeleka hiyo fainali.

Sasa, timu inajiandaa kumenyana na Uruguay au Colombia katika mchezo ambao unaweza kuwa wa mwisho kwa Di Maria na Messi.

Argentina itasafiri hadi Miami, Florida ambapo Messi anachezea klabu ya Inter Miami CF kucheza mechi ya fainali kwenye Uwanja wa Hard Rock Julai 14.

HABARI MICHEZO

# JOHN BOCCO ATUA RASMI JKT TANZANIA

Na Shufaa Lyimo

UONGOZI wa klabu ya JKT Tanzania, jana umemtangaza aliyekuwa nahodha wa klabu ya Simba, John Bocco, kuwa mchezaji wao kwa ajili ya Ligi Kuu msimu ujao.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Masau Bwire, alisema mbali na Boko vile vile wamefanya usajili wa wachezaji wengine ambao ni Abdurahim Seif Bausi kutoka klabu ya Uhamiaji ya Zanzibar, Charles Martin (Mtibwa Sugar), Denis Richard (KMC) na Karim Mfaume (Biashara United).

Wengine ni Elisha Japhet (Twalipo), Hamis Salum Hamis (KVZ), Kombo Hatibu (Coastal Union) pamoja na Wilson Nanau kutoka klabu ya TMA ya ligi ya Championship.

Pia uongozi huo umemtangaza Jemedary Said kuwa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo pamoja na ile ya wanawake, JKT Queens huku Hamady Ally akitangazwa kuwa Mkurugenzi wa benchi la ufundi wa timu hizo.

Alisema kutokana na mabadiliko waliyoyafanya wameteua kamati mbali mbali ikiwamo ile ya mratibu wa JKT Queen itakayoongozwa na Meja Ester Ryoba, huku JKT Tanzania ikiwa chini ya Stanley Joseph.

Huku Kamati ya Mashindano ikisimamiwa na Luteni Said Lobbe wakati Kamati ya Sheria ikisimamiwa na Kapteni Emmaculata Marunda.

Vile vile kwa upande wa Idara ya Masoko itaongozwa na Kapteni Spelatus Nyemela na Idara ya Habari na Mawasiliano itaendelea kuwa chini yake (Masau) ambapo mlezi wa timu hizo ni Bregedia Jenerali Hassan Mabena na Mwenyekiti wake atakuwa Geofrey Loyd Mvula.

Hata hivyo alisema Bodi ya Wakurugenzi itaongozwa na Luteni Kanali Javan Joseph, Luteni Ramadhan Salum pamoja na Meja Mohamed Ayoub Shamsama.

"Mabadiliko hayo tumeyafanya kwa lengo la kuimarisha kikosi chetu kuelekea mashindano ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara tuweze kushika nafasi za juu kwenye msimamo wa Ligi hiyo, alisema Bwire.

Aliongeza kuwa usajili waliofanya utaleta mapinduzi makubwa katika msimu huo na kuweka wazi malengo yao ni kufanya vema katika michezo yao yote ili wapate nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa.




# Gofu wanawake kushiriki mashindano ya Afrika

Na Shufaa Lyimo

TIMU ya Taifa ya Wanawake ya Mchezo wa Gofu inatarajiwa kushiriki mashindano ya ‚All African Challenge Trophy' yaliyopangwa kufanyika Novemba 28-30 nchini Morocco.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam hivi karibuni, Rais wa Chama cha Gofu cha Wanawake (TLGU), Queen Siraki, alisema timu hiyo inaendelea na mazoezi kuhakikisha inakwenda kuiwakilisha vema Tanzania.

"Kwa sasa timu yetu inaendelea kufanya mazoezi kila siku kwa lengo la kwenda kuitangaza nchi yetu kupitia mashindano hayo," alisema Queen.

Aidha, alisema timu hiyo imepanga kuondoka nchini Novemba 25 ili wachezaji wakazoee mazingira ya hali ya hewa nchini humo.

Alisema kila mchezaji ana morali ya juu jambo ambalo linampa matumaini makubwa ya kuibuka na ushindi kwenye michuano hiyo ambayo inatarajiwa kuwa na ushindani mkubwa.

Katika hatua nyingine, Queen alisema amefurahishwa na viwango vilivyoonyeshwa na wachezaji katika mashindano ya ‚Lugalo Vodacom Open' yaliyomalizika wiki iliyopita katika Klabu ya Gofu TPDF Lugalo jijini Dar es Salaam.

## Aziz Ki Yanga

INATOKA UK. 24

mkataba wake unamalizika msimu huu na wamekuwa katika nafasi nzuri kwa asilimia 60 kumbakisha, ingawa asilimia 40 zingine zinaweza kumfanya kuondoka kwa sababu kuna klabu zimekuwa zikiongea moja kwa moja na mchezaji.

Baada ya mazungumzo hayo, klabu kadhaa ikiwamo Mamelodi Sundowns na Orlando Pirates za Afrika Kusini, Simba na CR Belouizdad ya Algeria zilihusishwa kujitosa kumwania.

Katika kuonyesha kuwa mchezaji huyo amekuwa akiwindwa na klabu mbalimbali Afrika, baadhi ya vyombo vya habari vya nje, vilichapisha barua ya ofa ya CR Belouizdad iliyoonekana kuandikwa kwenda kwa mchezaji mwenyewe huku ikionyesha ofa watakayompa.

Mchezaji hiyo alisajiliwa na Yanga miaka miwili iliyopita baada ya kuonekana kwenye michuano ya Kombe ya Shirikisho wakati timu yake ya wakati huo, Asec Mimosas ilipocheza dhidi ya Simba mwaka 2022 baada ya kukutana kwenye kundi moja la michuano hiyo.

## Simba yaachana na Babacar, Lakred atua kambini Misri

INATOKA UK. 24

popata nafasi alijitoa kwa asilimia 100 kuhakikisha timu inapata ushindi, tunamtakia kila la heri katika maisha mapya ya soka nje ya Simba," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Katika hatua nyingine, golikipa namba moja kwa sasa wa klabu hiyo, Ayoub Lakred, ameungana na wenzake kambini nchini Misri kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa mashindano, huku kundi la pili pia likiwasili jana.

Kipa huyo ambaye hakusafiri na wenzake, aliwasili kambini hapo katika mji wa Ismailia akitokea kwao nchini Morocco alipokuwa amekwenda kwa mapumziko baada ya Ligi kumalizika.

Katika video zilizowekwa kwenye mitandao ya klabu hiyo zilimwonyesha kipa huyo akisalimia na wenzake, pia akiwa mmoja wa walioanza mazoezi ya ‚gym'.

Kulikuwa na wasiwasi kwa wanachama na mashabiki wa Simba kuhusu kipa huyo aliyeonyesha uwezo mkubwa msimu uliopita na kujizolea umaarufu mkubwa.

Wakati huo huo, kikosi cha pili kilichoondoka nchini jana kiliwasili salama kikiwa na wachezaji na benchi la ufundi likiongozwa na Kocha Mkuu, Faldu Davids na wasaidizi wake, Darian Wilken, Kocha wa magolikipa Wayne Sandilands, kocha wa viungo Riedoh Berdien na mchambuzi wa mechi, Mueez Kajee wote kutoka Afrika Kusini.


Michezo
Nipashe Alhamisi Julai 11, 2024

Meya amkataa Greenwood Marseille
UKURASA 21



# Aziz Ki aichagua Yanga

●●●Atoa neno kuwatoa hofu mashabiki licha ya kuwapo tetesi za kutakiwa na...



Aziz Ki

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

LICHA ya kuwapo kwa tetesi kuwa uwenda akaondoka katika klabu yake ya sasa, kiungo Aziz Ki jana ametoa kauri iliyoshusha 'presha' ya mashabiki wa Yanga.

Nyota huyo ambaye kumekuwa na tetesi za kutakiwa na klabu mbili za nje ya Tanzania, jana alisema bado yupo ndani ya Yanga.

Mchezaji huyo ambaye msimu uliopita alikuwa na mchango mkubwa wa kuifanya Yanga kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara na kuifikisha hatua ya robo fainali, amekuwa akihusishwa kuondoka baada ya mkataba wake kumalizika.

"Hallo wananchi, bado nipo," ilikuwa video fupi iliyowekwa na klabu hiyo jana kwenye mtandao wake wa kijamii ikimwonyesha mchezaji huyo akiongea mwenyewe juu ya kuendelea kuwapo kwenye kikosi hicho kwa msimu ujao, baada ya kuhusishwa kutaka kuondoka, taarifa zinasema nyota huyo wa Burkina Faso tayari amesaini mkataba wa miaka miwili kuendelea kuitumikia timu hiyo.

Tetesi za mchezaji huyo kuondoka zilishamiri na kushika kasi baada ya Rais wa Klabu hiyo, Hersi Said kunukuliwa akisema bado hawajamalizana na mchezaji huyo na kubainisha kuwa zipo timu zenye fedha zinazomuhitaji.

Akizungumza na waandishi wa habari wiki hii nchini Afrika Kusini, Hersi alisema walimsajili Aziz Ki miaka miwili iliyopita kutokea Asec Mimosas ya Ivory Coast ambapo

INAENDELEA UK. 23

## Simba yaachana na Babacar, Lakred atua kambini Misri

**Adam Fungamwango na Faustine Feliciane**

UONGOZI wa klabu ya Simba jana ulitoa taarifa ya kuachana na kiungo wake, Babacar Sarr baada ya kufikia makubaliano ya pande mbili.

Kiungo mkabaji alisajiliwa na Simba kwenye dirisha dogo la usajili msimu uliopita baada ya kumaliza mkataba wake kwenye klabu ya US Monastir ya Tunisia lakini ameonekana kutokwenda na kasi ya klabu hiyo.

"Tulikuwa na matumaini makubwa na Babacar kutokana na uwezo mkubwa alionao, lakini ameshindwa kuendana na kasi ya timu, katika kipindi chote cha miezi sita alichokuwa nasi, Babacar amekuwa mchezaji imara na mara zote ali-

INAENDELEA UK. 23



Baadhi ya wachezaji wa Simba wakiwa katika mazoezi jana kwenye kambi yao katika mji wa Ismailia, Misri kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu na mashindano ya kimataifa. **PICHA: SIMBA**

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >